**MACHO,** masikio bajeti ya kwanza ya Rais Samia leo

UKURASA 2



**RC** Shinyanga aapa kuiboresha kiuchumi akimulika utajiri wake

UKURASA 4


ama
ALHAMISI JUNI 10, 2021
AFYA NA MAZINGIRA
Ukurasa 12
SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI
Dk. Mpango: Suluhisho nishati mbadala
Ukurasa 14
KARNE TATU ZA KILIMO NGORO
Tija mazao bila mmomonyoko milimani, rutuba na kupendezesha ardhi Mbinga
SIKU YA HEDHI
'Wenye jambo lao' wapigana kutafuta haki iliko, shinikizo iwamo katika bajeti
Meya, Diwani watikisa kichwa 'ndiyo'
Na Yasmine Protace
Waziri Dk. Dorothy Gwajima; wizara yake ni muwajibikaji mkuu katika kutetea hedhi salama. PICHA: MTANDAO

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Juni 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580607

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# MASHEKHE UAMSHO

**VIONGOZI** wa dini watoa maombi maalum kwa Rais ... *Endelea Uk. 2*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na viongozi wa dini mbalimbali wakiongozwa na Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi (wa pili kulia), Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MEMKWA FURSA AJIRA KWA WALIMU**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri nchini...

**UKURASA WA 5**

**BIL. 1.5/- ZAKUSANYWA UKAGUZI MAGARI YA NJE**

SERIKALI imekusanya Sh. bilioni 1.5 kwa takribani siku 50 tangu ilipoanzisha utaratibu...

**UKURASA WA 16**

**MABASI 15 YAZUIWA KUSAFIRISHA ABIRIA**

JESHI la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, limeyazuia mabasi 12...


# Mbowe ataka tume ya ukweli, upatanishi

**ASHAURI** walioumiza wananchi waombe radhi hadharani... *Endelea Uk. 2*



## SERIKALI: MARUFUKU KUZUIA MAITI HOSPITALINI

UKURASA 3

**MICHEZO** **KARIA AZIDI KUPATA WAPINZANI URAIS TFF** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Mashekhe Uamsho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini Zanzibar wamemuomba Rais Dk. Hussein Mwinyi kuangalia suala la mashekhe wa Jumuiya ya Kiislam (Uamsho), ambao wako mahabusu kwa muda mrefu.

Wamesema ni vyema hatua zikachukuliwa kuangalia kama wana hatia au la badala ya kuendelea kusota rumande bila kujua hatima yao.

Ombi hilo lilitolewa na Katibu wa Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, wakati akizungumza na waandishi wa habari Ikulu, Zanzibar baada ya viongozi hao kufanya mazungumzo na Rais Dk. Mwinyi, Ikulu.

Alisema ni muda mrefu mashekhe hao wamekaa ndani na kuomba vyombo husika vikahakikishe mashekhe hao wanashughulikiwa suala lao, kama wataonekana wanahatia wahukumiwe na kama hawana hatia, busara itumike watolewe ili kila mmoja afaidike na matunda ya amani na utulivu uliopo nchini.

Alisema hivi sasa nchi ipo katika hali ya amani na utulivu na wananchi wake wapo pamoja na kila mmoja ana matumaini na serikali, kuwa ni vyema busara ikatumika kwa sababu mashekhe hao wameshakaa ndani kwa muda mrefu na imefika wakati sasa mamlaka inayohusika ikaliangalia suala hilo.

"Imefika wakati mamlaka zinazohusika kujaribu kuliangalia hili jambo kama mashekhe hao wahukumiwe na kama hawana hatia ni vyema busara ikatumika ili waendelee kufurahia matunda ya amani na utulivu katika nchi yao," alisema.

Katibu huyo alisema viongozi wa dini wataendelea kusimamia misingi ya dini ikiwamo kupendana, kuoneana imani, huruma na wataendelea kuhubiri amani na wananchi kuishi kwa upendo bila ya kubaguana.

Alisema viongozi wa dini wana haki zaidi ya kuzungumza ukweli na kubaki katika kulinda nidhamu ya dini.

Naye Katibu wa Viongozi wa Dini ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Maaskofu Zanzibar, Dickson Kaganga, alisema lengo la kukutana na Rais ni kumpongeza kwa hatua mbalimbali anazozichukua ikiwemo kushajihisha umoja, mshikamano na amani ya nchi.

Alisema tangu Dk. Mwinyi alipoingia madarakani migawanyiko ya kijamii na kisiasa imetoweka na hivi sasa wananchi wanafanya kazi zao kwa ushirikiano na upendo.

Alisema uongozi wake umeleta matumaini makubwa kwa wananchi wote bila ya kujali itikadi za kidini hivyo kuendelea kujitahidi ili matumaini hayo yazidi kufanikiwa.

Kadhalika katika mazungumzo yao walimshauri Dk. Mwinyi kutengeneza utoaji elimu kuhusu uchumi wa bluu ili wananchi wafahamu kwa sababu bado wananchi hawana uwelewa kuhusu uchumi huo.

"Sisi viongozi wa dini tunaunga mkono jitihada zote zinazofanywa na Dk. Mwinyi...tunafahamu kuwa wapo baadhi wanatamani turudi tulipotoka katika siasa za chuki na uhasama ambazo hazina maana hivyo tunawaasa waumini wote na wananchi wote kumuunga mkono rais katika hatua zake za kuleta maendeleo," alisema.

Kwa upande wake kiongozi wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Father Damas Aley Mfoi, alisema wamemshauri Rais Dk. Mwinyi kuwa na utaratibu pia kwa waumini wa dini ya Kikristo kuwapitia na kuwa nao pamoja katika ibada zao kama anavyofanya kwa waumini wa dini ya Kiislamu katika sala ya Ijumaa.

"Tunashukuru rais ametukubalia ombi letu na ametuahidi kuwa ataandaa utaratibu wa kuwa nasi katika ibada ya salamu yetu ya kila Jumapili kwa kutembelea makanisa ya waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini," alisema.

Alisema Rais Mwinyi ni msikivu na kwamba viongozi wa dini wapo pamoja na kuahidi kuendelea kumuunga mkono katika jitihada zake za kuiletea maendeleo Zanzibar.

# Bajeti ya kwanza ya Samia leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MACHO na masikio ya Watanzania yanatarajiwa kuelekezwa bungeni jijini Dodoma leo, wakati Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 itakapowasilishwa ili ijadiliwe na kupitishwa na chombo hicho.

Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki zinatarajiwa kuanika bajeti zake, Waziri wa Fedha na Mipango wa Tanzania, Dk. Mwigulu Nchemba akitarajiwa kuwasilisha bajeti ya Sh. trilioni 36.3, sawa na ongezeko la asilimia nne kulinganishwa na bajeti ya mwaka huu.

Bajeti inayowasilishwa leo ni ya kwanza chini ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyechukua uongozi wa nchi Machi 19, mwaka huu kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Mapendekezo yaliyotolewa kwenye ukomo wa bajeti, yalibainisha kuwa kati ya fedha hizo, asilimia asilimia 37 ya bajeti yote itaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi maendeleo.

Katika mapendekezo hayo ya awali, serikali inatarajiwa kutumia Sh. trilioni 10.7 (asilimia 29.5 ya bajeti yote) kulipa fedha madeni.

Miongoni mwa vipaumbele vya serikali vilivyotajwa kwenye mapendekezo ya awali ni kugharamia miradi ya kipaumbele na kimkakati, Deni la Serikali, mishahara ya watumishi, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, mpango wa elimu msingi bila ada na uendeshaji wa ofisi.

Katika mapendekezo yaliyotolewa kwenye wizara mbalimbali za kisekta, serikali inalenga kuipa sekta binafsi uzito mkubwa huku ikipendekeza utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwamo ya Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115, kuboresha Shirika la Ndege (ATCL) na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa.

Miradi mingine ya kielelezo ni pamoja na wa makaa ya mawe, Mchuchuma na Chuma - Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa (SGR) kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga.

Pia bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) na mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) mkoani Lindi.



Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa heshima za mwisho kwenye Jeneza lenye mwili wa mwanasiasa mkongwe, Marehemu Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, wakati wa misa ya kumwombea katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Petro Oysterbay, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mbowe amuomba Samia tume ya ukweli, upatanishi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amemshauri Rais Samia Suluhu Hassan, kuunda tume ya upatanishi, ukweli na maridhiano ili isikilize vilio vya Watanzania walioumizwa na kuteswa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Amesema hatua ya kuunda tume hiyo ni kutoa fursa na nafasi kwa watu kutoka makundi mbalimbali kujitokeza kusema ukweli Ili waliofanya makosa waombe radhi ili matukio hayo yasijirudie.

Mbowe alitoa ombi hilo wakati wa mkutano wa Baraza la Mashauriano wa CHADEMA Mkoa wa Morogoro uliowashirikisha viongozi wa chama hicho kutoka majimbo 11 ya uchaguzi ya mkoa huo.

Alisema baada ya kuundwa tume hiyo na watu kupewa nafasi ya kuwasilisha madhila walioyapata, itasaidia waliofanya makosa waliombe radhi Taifa ili kufikia maridhiano ya pamoja.

Kwa mujibu wa Mbowe, yapo makundi ya wakulima, wafugaji, wavuvi, viongozi wa dini ambao wameumizwa na baadhi ya viongozi waliokuwa madarakani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Alisema kukamatwa kwa aliyekuwa kiongozi mmoja wa serikali hivi karibuni na kufikishwa mahakamani kwa tuhuma mbalimbali, sio suluhisho la vilio vya Watanzania wengi waliotеswa na baadhi ya viongozi waliokuwa serikalini kipindi hicho.

" Wapo viongozi na watumishi kutoka taasisi mbalimbali, na sehemu nyingine wamewaumiza sana Watanzania katika kipindi hicho cha miaka mitano iliyopita wajitokeze kuliomba radhi taifa hili ili tuishi kwa maridhiano," alisema Mbowe.

Alisema hakuna sababu ya kukwepa kuundwa tume hiyo kwa kuwa waliofanya hivyo mpaka sasa wapo katika serikali na wanaendelea kufanya kazi bila shaka yoyote.

HABARI KITAIFA

# Serikali yapiga marufuku maiti kuzuiwa hospitalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imepiga marufuku hospitali na vituo vya afya nchini kuzuia maiti na badala yake imeagiza kuwapo utaratibu wa ulipaji wa gharama za matibabu kadiri mgonjwa anavyopata huduma.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyotoa juzi alipokuwa akizungumza na wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kuagiza kuwekwa mpango mzuri ambao hautasababisha kuzuia maiti.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kikao cha siku tatu cha kujadili na kufanyia kazi maeneo ya kimkakati na maagizo ambayo yametolewa na viongozi wa kitaifa.

Alisema ni mafuruku kiongozi au mtu yeyote wa mochwari kuzuia maiti kwa kisingizio cha kutolipwa gharama za matibabu na kutaka hospitali ziweke utaratibu wa kulipia kadri mgonjwa anavyopata huduma.

"Tumetoa mwongozo na barua tumeshapeleka tangu jana (juzi) kwenye vituo vyote kuwakumbusha hili. Tusije tukasikia tena mwananchi analalamika marehemu wake amezuiwa kutoka mochuwari katika ardhi hii ya Tanzania," alisema.

"Tuweke tu utaratibu mzuri, anavyotibiwa mgonjwa kama kuna gharama za kuchangia zilipwe kupitia ndugu zake. Hatusemi watu wasilipe lakini tusilimbikize deni, uwekwe utaratibu wa kulipa wakati akiwa anapata huduma ili isitokee maiti kudaiwa pindi mgonjwa anapofariki dunia," aliongeza.

Alisema tayari mwongozo huo umeanza kutumika, hivyo serikali haitarajii kusikia kiongozi au mtu yeyote wa mochwari au hospitali kuzuia maiti.

"Kuna utaratibu wa kushughulikia watu wasio na uwezo na kuna mwongozo kwa makundi ambayo yana msamaha wa moja kwa moja kisera ambayo huwa tunayatambua tunapotoa huduma, hata ikitokea mgonjwa amefariki dunia husamehewa.

Kuna kamati za misamaha kwenye hospitali zetu na vituo huwa zinaangalia huyu mtu kweli hana uwezo? Zikijiridhisha kulingana na sera anasamehewa," alisisitiza.

Prof. Makubi alisema serikali haitaki maiti yoyote izuiwe ama iwe ya msamaha au si ya msamaha na kutaka kuruhusu maiti izikwe na madeni yabaki kudaiwa kwa familia kwa utaratibu utakaowekwa.

Kuhusu tahadhari za ugonjwa wa Corona, Prof.Makubi alisisitiza tahadhari ziendelee kuchukuliwa na wananchi katika kukabiliana na ugonjwa huo kwa kunawa mikono kwa sabuni na ikibidi kwenye mikusanyiko kuvaa barakoa.

Alitoa wito kwa viongozi wa dini nchini kuhakikisha wanawaomba waumini kuchukua tahadhali dhidi ya ugonjwa huo bila kuwapa hofu wananchi.

# MEMKWA fursa ajira kwa walimu

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri nchini, kufufua madarasa ya Mpango kwa Elimu Maalum kwa Waliokosa (MEMKWA) na walimu waliohitimu ualimu ngazi ya cheti, stashahada na wanaojitolea, watumiwe kufundisha.

Ameagiza halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuwalipa walimu hao na kwamba miundombinu itakayotumika ni ambayo inatumika kutoa elimu kwa sasa.

Majaliwa aliyasema hayo jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alipozindua kongamano la kimataifa kuadhimisha miaka 50 ya elimu ya watu wazima nchini.

"Fedha zitengwe za walimu watakaofundisha madarasa hayo, tuna wanafunzi waliohitimu diploma, ngazi ya cheti ya ualimu, hawajaingia katika mfumo rasmi.

"Watumike kufundisha, itumike miudombinu ya shule iliyopo kufundishia watu wazima," Majaliwa aliagiza.

Alisema elimu ya watu wazima kwa asilimia 60 hadi 70 waliopata elimu ya kufuta ujinga wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), walitoa mwamko kwa watoto wao kuanza shule, kufuatilia maendeleo yao na kuhakikisha wanahitimu. Majaliwa alisema wazazi waliopata elimu hiyo kwa asilimia 50 wameelimika kuhusu masuala ya afya na lishe, na hivi sasa watoto wameelimika kufanya vizuri darasani huku wakitoa ushirikiano kwa walimu.

"Baada ya Uhuru mwaka 1961, kwa asilimia 80 nchi nyingi ikiwamo Tanzania kuna wakati ilikuwa watu wazima walikuwa hawajui KKK, ilikuwa lazima kuanzishwa kampeni hii iliyoanzishwa na Baba wa Taifa.

"Kwa miongo kadhaa elimu imeleta manufaa na ili kufikia uchumi wa juu inahitajika elimu na ujuzi wa kila mmoja kuimarisha kipato cha kila mmoja na taifa," alisema. Waziri Mkuu alisema mafanikio ya miaka 50 ya elimu hiyo ni mengi ikiwamo kukamilisha ndoto za watu wazima, ambao hawakuwahi kudhani wataweza kufikia elimu ya juu kutokana na vigezo vya kujiunga, majukumu ya kikazi pamoja na familia.

"Elimu ya watu hakika imefanya watu wazima wengi kufanikiwa na hadi kufikia Chuo Kikuu Huria (OPEN) ambacho kilianzishwa mwaka 1993.

"Elimu ya watu wazima inachangia pakubwa katika kufufua ujuzi na kila nyanja inahitaji maarifa ya watu wazima, rasilimali fedha itengwe kusaidia mpango huu," aliagiza.

Alisema kuhuisha kwa elimu hiyo hivi sasa kumekuja wakati mwafaka ili kufikia uchumi wa juu ambao unahitajika mchango na nguvu ya kila mmoja ikiwamo watu wazima na kwamba ujuzi unaopatikana katika mfumo rasmi na usio rasmi, utatambuliwa na serikali.

Majaliwa alisema kuna wakati wazazi au walezi husita kuwanunulia vifaa vya shule watoto wao wakidhani ni kazi ya serikali, hivyo kundi la wazazi ambalo limepata elimu ya watu wazima husaidia kujua umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuwa tayari kuchangia elimu.

Alisema Tanzania ilitambulika duniani kwa kufuta ujinga na kuongeza kiwango cha KKK kutoka asilimia 15 mwaka 1961 hadi asilimia 61 mwaka 1975, huku mwaka 1986 kiwango cha uelewa kikiongezeka hadi asilimia 90.4.

Majaliwa alisema mafanikio ya elimu hiyo pia yalitokana na lugha iliyotumika kufundishia ambayo ni Kiswahili, iliyosaidia kufundisha watu wote na pia kukikuza Kiswahili na kupewa tuzo na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Katika maagizo mengine, Majaliwa alizitaka halmashauri zote kuandaa kanzidata ya waliosoma na kuhitimu ili kubaini mafanikio kwa kila eneo nchini, wakuu mikoa kufungua madarasa, utafiti kufanyika ili elimu ya watu wazima iwe ya tija na wizara isijikite kutoa elimu ya mfumo rasmi pekee bali hata usio rasmi, ikiwamo ufundi.




MAKALA MAALUM

# RC aumulika utajiri wa madini, mifugo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati akisalimiana na baadhi ya viongozi wa dini alipowasili katika ofisi za mkuu wa mkoa huo.

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, ameweka bayana mikakati yake ya utendaji kazi mkoani humo, ili kuubadilisha kiuchumi kuendana na utajiri wa madini na mifugo uliopo.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe ofisini kwake mjini Shinyanga juzi, Dk. Sengati alisema adhima yake kubwa katika mkoa huo ni kuubadilisha kiuchumi.

Kiongozi huyo alisema mkakati huo unakwenda sambamba na kuweka kituo kikubwa cha biashara ukanda wa maziwa ambacho kitakuwa wilayani Kahama.

Alisema mkoa huo una utajiri mkubwa wa madini na mifugo mingi, lakini ukitazama hali yake kiuchumi, haiendani na rasilimali hizo, hivyo katika utendaji wake wa kazi atahakikisha unaubadilisha kiuchumi na kuboresha maisha ya wananchi wake, hasa kwenye ujenzi wa nyumba bora.

"Vipaumbele vyangu katika mkoa huu wa Shinyanga ni kukuza kiuchumi, kuimarisha ulinzi na usalama, kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato na kubuni vyanzo vipya, kusimamia matumizi ya mapato yaendane na mipango, kuvutia wawekezaji na kuwatengea maeneo pamoja na kuondoa urasimu.

"Pia nitaboresha mazingira ya wakulima, walime kwa mikataba na kuuza mazao yao kwa stakabadhi gharani ili kilimo chao kiwe na tija na kuinuka kiuchumi," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Sengati alisema watapanga mipango bora ya matumizi ya ardhi na maeneo kwa ajili ya machinga, ili wawe na maeneo maalum ya kufanyia biashara na kukuza mitaji yao kupitia mikopo ya halmashauri.

Kabla ya kutua Shinyanga, Dk. Sengati alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora.

**USULI**

Tovuti rasmi ya Mkoa wa Shinyanga inabainisha ulikuwa ni sehemu ya Mkoa wa Ziwa (Lake Province) mpaka mwaka 1963 ulipoanzishwa rasmi ukiwa na wilaya tatu za Maswa, Shinyanga na Kahama iliyomegwa kutoka Mkoa wa Tabora.

Kuanzia mwaka 1972 hadi mwaka 1982, Serikali ya Mkoa ilikuwa katika mfumo wa Madaraka Mikoani ambapo vyama vya ushirika, utemi na serikali za mitaa zilifutwa.

Mkoa wa Shinyanga uliendelea kukua ambapo maeneo mapya ya utawala yalianzishwa na kufikia wilaya saba ambazo ni Kahama, Bukombe, Maswa, Kishapu, Bariadi, Meatu na Shinyanga.

Pia, kuanzia mwaka 2012 kutokana na mkoa kukidhi vigezo muhimu vya kitaifa vya uanzishaji maeneo mapya ya utawala, serikali ilifanya uamuzi wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala ambapo mikoa mipya ya Simiyu na Geita ilianzishwa ikiwa imemega baadhi ya wilaya za Mkoa wa Shinyanga.

Wilaya za Bariadi, Maswa na Meatu zilimegwa kuanzisha Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Bukombe ilipelekwa Mkoa mpya wa Geita.

Mkoa wa Shinyanga uliongeza maeneo ya kiutawala kwa kuanzisha Halmashauri mpya za Kahama Mji mwaka 2012, Msalala na Ushetu mwaka 2013 ambazo zilitokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Kahama.

Uamuzi huo wa Serikali unalenga kuboresha huduma za kiutawala na maendeleo ili wananchi wapate kwa karibu zaidi.

Kijiografia, Mkoa wa Shinyanga uko kaskazini magharibi mwa Tanzania na kusini mwa Ziwa Victoria, ukipakana na mikoa ya Mwanza, Simiyu na Geita kwa upande wa kaskazini, upande wa mashariki Mkoa wa Simiyu, upande wa magharibi Mkoa wa Geita na upande wa kusini Mkoa wa Tabora.

Mkoa wa Shinyanga wenye eneo la kilometa za mraba 18,555, hadi sasa umeongozwa na wakuu wa mikoa 22.

Fursa za uwekezaji zilizopo Shinyanga ni pamoja na bandari kavu, madini, kilimo, mifugo na vivutio vya utalii.

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ilibaini Shinyanga ilikuwa na wakazi 1,534,808 (milioni 1.5).




Shinyanga ina hazina kubwa ya madini hasa almasi na dhahabu.



Mifugo ni sehemu ya fursa nyingi za uwekezaji mkoani Shinyanga.

HABARI KITAIFA

# Samia ateua mrithi wa Msigwa Ikulu




**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Jaffar Haniu (pichani) kuwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema uteuzi huo ulianza rasmi jana.

Kabla ya uteuzi huo, Haniu alikuwa Mtendaji Mkuu wa vyombo vya habari vya Africa Media Group Limited.

Haniu anachukua nafasi ya Gerson Msigwa ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali. Aidha, Haniu ambaye kitaaluma ni mwanahabari, amewahi kufanya kazi kwa miaka kadhaa katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) tangu wakati huo ikiitwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

Pia kuanzia katikati ya miaka ya 2010, aliwahi kufanya kazi katika Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu katika nafasi kadhaa ikiwamo ya naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano katika ofisi hiyo.

# Bil. 1.5/- zakusanywa ukaguzi magari ya nje

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekusanya Sh. bilioni 1.5 kwa takribani siku 50 tangu ilipoanzisha utaratibu wa magari kutoka nje kukaguliwa nchini.

Kiasi hicho kimekusanywa baada ya Shirika la Viwango (TBS) kukagua magari 4,779 yanayoagizwa kutoka nje.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Udhibiti wa Ubora wa TBS, Mhandisi Said Mkwawa, wakati wa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari juu ya najukumu ya Shirika hilo.

Alisema utaratibu wa kukagua magari yanayoagizwa kutoka nje umeongeza wigo wa makusanyo ya mapato ya serikali, kwa sababu awali wakati magari yalipokuwa yakikaguliwa nje, serikali ilikuwa inapata Sh. milioni 600 tu kwa mwezi.

Alifafanua kuwa fedha zinazokusanywa zinapokelewa kwa kutumia mfumo rasmi wa malipo ya serikali, na kwamba TBS haipokei fedha taslimu.

Alieleza kuwa asilimia 85 ya hitilafu wanazozibaini kwenye ukaguzi ni kwenye matairi, taa na mambo mengine madogo.

Kadhalika, alisema TBS imeanza mchakato kuagiza mitambo ya kisasa kwa ajili ya ukaguzi wa magari na kwamba zimeagizwa Ujerumani kwa gharama ya Sh. bilioni 3. Alisema zitawezesha kukaguliwa magari 1,200 kwa siku kutoka magari 480.

Meneja wa TEHAMA, JabirAbdi, alisema utaratibu mpya umesaidia kutoa ajira vijana kwenye gereji kwa ambazo magari yanayokutwa na hitilafu yanafanyiwa matengenezo pamoja na kuwaongezea kipato wenye maduka ya kuuza vifaa vya magari.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, aliwaonya wanaotaka kuagiza magari kutowatumia watu ambao hawana kampuni ili kuepuka gharama kubwa ambazo wataingia kuyafanyia matengenezo wenyewe, badala yake wawatumie mawakala wenye kampuni.




NATIONAL INVESTMENTS PLC



TANGAZO LA KUHAMA KWA OFISI ZA NICOL

KATIKA JITIHADA ZA KUENDELEA KUBORESHA MAWASILIANO NA WANAHISA WETU, KAMPUNI YA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL) TUNAPENDA KUWATAARIFU WANAHISA NA WANANCHI KWA UJUMLA KUWA TUMEHAMISHA OFISI ZETU.

OFISI ZETU ZA NICOL ZILIZOKUWEPO MIKOCHENI B, 11 SERENGETI ROAD ZIMEHAMIA POSTA MPYA MTAA WA MIRAMBO (50 MIRAMBO STREET) GHOROFA YA TATU JENGO LA "MIRAMBO HOUSE", ZILIPO OFISI ZA BENKI YA DUNIA (WORD BANK OFFICE).

HUDUMA ZOTE ZA NICOL ZITAENDELEA KUTOLEWA KATIKA OFISI ZETU MPYA, KAMPUNI INAOMBA RADHI KAMA PATATOKEA USUMBUFU WOWOTE UTAKAOSABABISHWA NA MABADILIKO HAYA.

KUTOKANA NA MABADILIKO HAYO, MAWASILIANO NASI YATAFANYIKA KUPITIA ANUANI ZIFUATAZO

**NATIONAL INVESTMENTS PLC**
POSTA MPYA, 50 MIRAMBO STREET,
MIRAMBO HOUSE, 3RD FLOOR,
P O BOX 7465,
DAR ES SALAAM.
**Phone 0682720679 / 25522 2701436**
**Email- invest@nicol.co.tz**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Uchaguzi Tahasusi umulikwe vizuri

**HIVI** karibuni kumezuka mjadala mtandaoni juu ya tahasusi wanafunzi alizopangiwa na shule, kwa baadhi ya wazazi, wanafunzi kudai walichopangiwa sicho alichojaza kwenye mfumo maalumu, na serikali ikisema amepangiwa kwa kadri ya chaguo lao.

Malalamiko yalitolewa na wazazi mtandaoni, kutuma ujumbe mfupi wa maandishi huku mwanafunzi mmoja akivaa mabango yenye ujumbe na kukaa juani kufikisha ujumbe wa kutoridhika na tahasusi pamoja na shule aliyopangiwa kuendelea na kidato cha tano.

Kutokana na malalamiko hayo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitumia mitandao yake ya kijamii kujibu kwa mifano hoja mbalimbali za wazazi, na kusisitiza kuwa walichopangiwa wanafunzi ndicho walichochagua katika chaguo la kwanza hadi la tano.

Wapo wazazi waliolalamika kuwa watoto wao walichagua kuendelea na kidato cha tano, licha ya kuwa na ufaulu wa daraja la kwanza, lakini bado walipangiwa kujiunga na vyuo vya diploma.

Pia, wapo waliolalamika kupangiwa shule na tahasusi ambazo hawakuchagua na kwenye mitandao ya kijamii alijaribu kumwonyesha waziri kuwa kilichofanyika sicho.

Kimsingi licha ya ufafanuzi wa serikali bado inaonyesha kuna tatizo mahali hasa katika kuchagua na kupanga wanafunzi, kwa kuwa bado inafikirisha aliyepata daraja la kwanza imekuwaje anapangiwa kwenda chuo wakati hakupenda kwenda huko.

Lakini mara nyingi imekuwa ndiyo utaratibu kwamba wenye ufaulu mdogo wanakwenda kusoma sayansi, huku wenye ufaulu mkubwa wakienda kusoma ualimu.

Pia, kuna dhana kuwa ambaye hakuendelea na kidato cha tano maana yake hakufanya vizuri kwenye mitihani yake, na hili ni muhimu sana likatolewa ufafanuzi kwa kuwa limesababisha matabaka kwenye elimu hadi ajira.

Inaaminika kuwa mwanafunzi aliyesoma hadi kidato cha sita ni bora zaidi ya aliyesoma diploma kisha akaenda chuo kikuu, na hii inadhihirisha kuwa ni lazima mfumo wa elimu utazamwe upya, kwa kuhakikisha unapika wataalam bora kwa taifa.

Kama ambaye hajafanya vizuri ndiye anapangiwa kusoma ualimu maana yake tumefundishwa, wanafundishwa na watafundishwa na watu ambao hawajakidhi matakwa sahihi, na kama ndiyo utaratibu maana yake aliyefeli ndiye anapaswa kuandaa mtaalam ambaye atakwenda kufundisha waliofanya vizuri.

Lakini ni muhimu huu utaratibu wa kuchagua cha kusomea ukatoa nafasi kwa wanafunzi wenyewe baada ya kuelimishwa vyema kutambua ni nini anakwenda kusomea, atafanyakazi gani na asipangiwe kingine ambacho hatakiweza.

Madhara ya kupangiwa kwa sababu ya utaratibu au wazazi kutaka mtoto wao awe kama fulani ni makubwa kwa kuwa kuna hatari kubwa ya kuwa na wataalam ambao wamesomea walichosomea kama njia ya kupita na siyo kwamba wanapenda kazi husika.

Mathalani, kuna wakati kulikuwa na wimbi la wanafunzi kujiunga na ualimu kwa kuwa ilikuwa njia ya kupita ili kupata ajira kwa haraka na baada ya hapo anaomba ruhusa kwenda masomoni kusomea kitu kingine na baadaye harudi kituo cha kazi, lakini kwa muda wote anaendelea kulipwa mshahara.

Ni muhimu sana serikali ikaangalia suala la upangaji wa tahasusi ili kuhakikisha mwanafunzi anasomea kile anachokipenda, na kuwe na ufafanuzi mzuri wa nani anayetahili kusoma diploma na anayestahili kuendelea na kidato cha tano, ili kuondoa matabaka ya kwamba kuna aliyebora na wasiobora ambao wote watakutana vyuo vikuu.

Je inapofika kwenye ajira kinachoangaliwa ni njia uliyopita kupata utaalam fulani au ni kiwango cha ufaulu wako na sifa inayokufanya ubaki kazini? Yote haya yafafanuliwe ili wanafunzi akipangiwa vyuo wazazi na wanafunzi wasione shida.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Vifo hivi vitushitue kuwa makini utumiaji tumbaku

**WAVUTAJI** wa sigara, sasa ni wazi kwamba wanapaswa kufikiria upya starehe yao hiyo na ikiwezekana wachukue hatua ya kuachana nayo, kwa kutafuta mbadala ili kuepuka madhara ya kiafya wanayoweza kuyapata.

Hiyo ni kwa sababu inakadiriwa watu milioni sita, hufariki kila mwaka duniani, kutokana na matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, zikiwamo sigara na shisha au asiye mvutaji kujikuta anavuta moshi kutoka kwa mvutaji

Inaelezwa katika mazingira hayo asilimia 28 ya watoto wanapoteza maisha, kati yao wanawake asilimia sita na wanaume asilimia 12. Inakadiriwa hadi kufikia mwaka 2030, vifo vitokanavyo na tumbaku vitaongezeka na kufika zaidi ya milioni nane kwa mwaka.

Licha ya watu kufariki dunia kwa kutumia tumbaku na kuvuta moshi kutoka kwa mtumiaji madhara yanayowapata waathirika ni pamoja na kupata magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo saratani, magonjwa ya njia ya hewa.

Magonjwa mengine yanayotajwa, ni pamoja na mapafu na kisukari na yanayoathiri moyo, mishipa ya damu na kuongeza hatari ya kupata shinikizo la juu la damu.

Hivi sasa nchini, kunatajwa wastani asilimia 14 ya Watanzania wanatumia tumbaku na kwamba idadi ya wanaoathirika kutokana na moshi wa tumbaku kutoka kwa wavutaji inaongezeka.

Kutokana na athari hizo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anakiri tatizo na anahimiza serikali inaendelea kulipiga vita kupitia wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007.

Ni sera ambayo sehemu ya maudhui yake inalenga kuhudumia magonjwa yasiyoambukizwa kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO,) ambalo limekuwa likifanya jitihada mbalimbali za kudhibiti matumizi ya bidhaa za tumbaku.

**Ufafanuzi wake uko kwenye maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Kupinga Matumizi ya Tumbaku, kwamba hadi sasa serikali inaendelea kusisitiza kuacha utumiaji wa bidhaa za tumbaku iitwayo 'shisha.'**

Ufafanuzi wake uko kwenye maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Kupinga Matumizi ya Tumbaku, kwamba hadi sasa serikali inaendelea kusisitiza kuacha utumiaji wa bidhaa za tumbaku iitwayo 'shisha.'

Kwa kuwa ni wazi kwamba bidhaa hiyo ina madhara kwa afya za watu, basi kuna haja kila mmoja wetu kuanzia kwa wavutaji na wanaovutoshwa tumbaku kujiongeza ili waweze kulinda afya zao.

Hiyo inafanya umuhimu wa jamii kuongeza uelewa kwenye madhara yanayoweza kupatikana kutokana na matumizi ya tumbaku au kuwa karibu na mtu anayetumia kilevi hicho.

Jinsi mazingira ya uvutaji yalivyo nchini, baadhi ya watumiaji tumbaku wamekuwa wakivuta kwenye mikusanyiko ya watu, hata inawezekana watakuwa wameumiza wengine bila ya kujua au wanaovutisha nao bila kujua.

Elimu ni muhimu kwenye janga hilo, ambalo linatajwa kuchangia vifo milioni sita kwa mwaka, ili jamii iweze kuwa makini badala ya kuendelea kushuhudia watu wakivutishwa tumbaku bila kujua madhara yake.

Inasikitisha kusikia matumizi ya tumbaku yanaangamiza maisha ya wavutaji na wanaovutishwa, hivyo ipo haja ya kuelimisha umma wa Watanzania kuhusu madhara, pia kuepuka matangazo ya kuhamasisha uvutaji.

Katika pakti za sigara zimeandikwa tahadhari, ambayao ikiendana na elimu maradufu kwa umma, inaweza kusaidia kutimiza kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu isemayo "dhamiria kuacha kutumia tumbaku na bidhaa zake."

Vilevile itapendeza iwapo ushauri wa wadau wa kupinga matumizi ya tumbaku utazingatiwa, ambao ni kutaka kutafuta mazao mengine mbadala wa zao hilo.

Karanga, chai, ufuta na alizeti ni miongoni mwa mazao ambayo yanaweza kuwa mbadala ya tumbaku, japo moja kati yao na yana soko kubwa la kuweza kuiingiza serikali fedha za kigeni.

# Vijana wapata fursa mikopo ya bodaboda

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDUMA

VIJANA wanaojishughulisha na shughuli za iendeshaji bodaboda na majaji wamepata fursa ya mikopo.

Fursa hiyo imetokana na Benki ya NMB kuzindua mikopo ya pikipiki za miguu miwili na zile za miguu mitatu kwa Kanda ya Nyanda za Juu (NMB MastaBoda Loan ), ambayo ni maalumu kwa vijana wanaojishughulisha na usafirishaji wa abiria kupitia pikipiki za miguu miwili na pikipiki za miguu mitatu.

Katika uzinduzi huo ambao ulifanyika mjini Tunduma mkoani Songwe, Meneja wa kanda hiyo, Straton Chilongola, alisema mikopo inayotolewa ni nafuu kwa vijana ambapo sharti ni kuwa na akaunti katika benki ya NMB.

Alisema uzinduzi wa mikopo hiyo kwa kundi la vijana ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali yaliyotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Sera, Bunge na Watu wenye Ulemavu), Jenister Mhagama Oktoba mwaka 2019 wakati wa uzinduzi wa kampeni ya NMB Mastaboda iliyokuwa na lengo la kuwaunganisha vijana wa boda boda kwenye mfumo wa malipo kwa kutumia Mastercard.

Alisema kuwa NMB imeanzisha mpango huo ili kuunga mkono juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuchangia kutoa suluhisho la ajira kwa vijana na kuwawezesha kuingia kwenye mfumo rasmi wa kibenki kwa maslahi mapana ya kukuza maendeleo ya nchi.

Mkuu wa mkoa huo, Brigeria Jenerali Wilbert Ibuge, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa kampeni hiyo, aliipongeza NMB kuwakutanisha vijana hao na kutoa fursa ya mikopo kwani kupitia mfumo huo wanatoa ajira kwa vijana, huku akiiomba benki hiyo kupunguza riba na kuongeza muda wa mkopo ili wakopaji waweze kuimudu vema na wengi waweze kunufaika zaidi.

Mgumba amewataka waendesha pikipiki kuwa na nidhamu ya fedha za mkopo na vijana wengi watunze kumbukumbu zao kwa kufungua akaunti na watambuliwe pia kukuza uchumi wa Taifa. Vijana zaidi ya 200 waliohudhuria hafla hiyo walieleza kufurahia mpango huo wakisema ni afiki kwa kuwa riba ni ndogo na wao watamiliki vyombo hivyo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa bodaboda na bajaj jijini Dar es salaam, Michael Masawe, alisema tangu kuanza mfumo huu NMB imewawezesha vijana wengi kunufaika kwa kumiliki pikipiki zaidi ya moja.



Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede akitoa ufafanuzi kuhusu maswali yaliyoulizwa na wabunge kwenye semina ya siku moja iliyofanyika ukumbi wa Msekwa Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Sendiga aanza na hoja za CAG

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameagiza hatua kali zichukuliwe dhidi ya watumishi waliosababisha kuwapo hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za Sh. milioni 107 kutopelekwa benki.

Pia, amewataka watumishi kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na weledi.

Akizungumza jana kwenye kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Kilolo, alisema pamoja na ushirikiano mkubwa anaoupata ndani ya mkoa anataka uende na uwajibikaji kwa kila mmoja.

"Naomba niwaeleze wazi nitakuwa mkali sana kwa mtumishi asiyewajibika kwenye eneo lake kwa sura mimi ni mpole sana ila kwa sura yangu hii nitakemea pale ambapo mtumishi hatawajibika," alisema.

Sendiga ambaye amekuja na kaulimbiu ya 'Uwajibikaji rafiki wa maendeleo' akiwa na maana ya kila mmoja atawajibika kufanya kazi, alisema katika uongozi wake hatapenda kuona halmashauri hiyo inaendelea kupata hati yenye mashaka. Halmashauri hiyo ilipata hati hiyo kutokana na miamala ya Sh. milioni 34 na kukosekana kwa taarifa sahihi ya fedha kiasi cha Sh. milioni 107 kutojulikana kama zilikwenda benki au la.

Aidha, alitaka uwajibikaji na kuhakikisha fedha zinakusanywa na kupelekwa benki kwa mujibu wa taratibu, ili kuepusha upotevu wa fedha. "Mkurugenzi naomba kukuagiza halmashauri kuongeza umakini ili hoja kama hizo za Mkaguzi wa Hesabu za Serikali zisiwepo tena ikitokea tena tutamsaka mmoja baada ya mwingine na kuchukua hatua kali dhidi yake," alisema Sendiga.

Pia, aliagiza kurejeshwa kwa Sh. milioni 79 zilizokopeshwa kwa vikundi vya wajasiriamali ili kuondoa hoja kwa mkaguzi na kukopesha wananchi wengine.

# Walimu, wanafunzi watumia choo kimoja

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALIMU katika Shule ya Msingi Mwamagunguli 'A' iliyoko Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, wanajisaidia choo kimoja na wanafunzi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwamagunguli, Adam Bega, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shule hiyo.

Alisema shule ina walimu wanane na wanafunzi 412, ambao kwa sasa wanatumia choo kimoja chenye matundu manne, kitendo ambacho siyo sahihi kwa afya.

"Katika choo hiki tumegawana matundu, walimu tunatumia tundu moja, wasichana moja na wavulana mawili, lakini kinidhamu siyo sahihi mwalimu kupishana na mwanafunzi chooni," alisema Bega.

"Tunaomba tujengewe choo sisi walimu hapa shuleni, tunashukuru sasa hivi kuna wafadhili kutoka Shirika la Tuthubutu Afrika Intiatives, wanajenga choo matundu manane kwa ajili ya wasichana jambo ambalo ni jema," aliongeza.

Alisema choo cha shule hiyo kwa sasa hakifai tena kwa matumizi kutokana na ubovu na kwamba wapo kwenye hatari ya kupatwa na magonjwa ya mlipuko.

Naye Diwani wa Kolandoto, Mussa Andrew, alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, tayari wameshaingiza kwenye mpango wa ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwamo vyoo.


**JAMHURI Y A MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA.87 YA 2021**
**S&C GINNING COMPANY LIMITED………………MDAI**
**NBCL DISTRIBUTION LIMITED……………..................MDAI**
**DHIDI YA**
**BHANJI CARGO AND HAULIERS LIMITED………..**
**MDAIWA**
**KWA.**
**BHANJI CARGO AND HAULIERS LIMITED**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameeleza katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii,kwahiyo mnatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 15 mwezi 6 mwaka 2021 saa mbili (2:00) kamili asubuhi.kwakua siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama leo tarehe 8 mwezi wa 6 /2021.

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA KINONDONI KIVUKONI**

# Kampeni elimu kodi yashika kasi

**Na Mwandishi Wetu,** KASULU

WAFANYABIASHARA wilayani Kasulu mkoani Kigoma wameifurahia kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea kutolewa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA), wakibainisha wamejua mambo mengi ya kodi tofauti na awali.

Jana wafanyabiashara hao waliomba elimu hiyo itolewe mara kwa mara ili kuongeza uelewa zaidi wa masuala ya kodi kwa sababu wafanyabiashara wengi huanza biashara bila kuwa na elimu ya masuala ya kodi.

"Mimi binafsi elimu hii ya kodi imenipa kujiamini hususani katika suala zima la makadirio kwa sababu nilikuwa ninakwenda kukadiriwa kodi bila kuwa na uelewa wa namna TRA inavyokokotoa makadirio yangu," alisema Santos Yona, mfanyabiashara wa vifaa vya umeme Kasulu mjini.

Yona alisema kuwa kupitia elimu ya kodi aliyoipata, amefahamu lengo la TRA ni kutaka yeye akue kibiashara ili aendelee kuchangia zaidi kwenye maendeleo ya nchi yake.

"Kitu kingine ni kwamba elimu ya kodi niliyoipata imenifumbua macho na kujua kumbe TRA ina lengo zuri na sisi wafanyabiashara maana wanataka tuongezeke kibiashara ili tuchangie kwenye ujenzi wa nchi yetu," alisema.

Emakulatha Cosmas, mfanyabiashara wa duka la vitenge mjini Kasulu, aliishukuru TRA kwa kuwapatia elimu ya kodi hususani katika utunzaji wa kumbukumbu ambao ulikuwa ukimtatiza hapo awali.

"Kusema ukweli mimi nilikuwa sina elimu ya utunzaji wa kumbukumbu, ninashukuru leo nimetembelewa dukani kwangu na kupewa elimu hii.

"Sasa nimejua kwamba ninatakiwa kuandika ununuzi, mauzo, faida na matumizi yangu ya biashara kama nilivyoelekezwa," alisema Emakulatha.

Kaimu Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Rose Mahendeka, ambaye pia ni kiongozi wa timu inayoelimisha walipakodi wilayani humo, alisema mipango yao inakwenda vizuri na mwitikio wa wafanyabiashara ni mkubwa.

"Kwa kweli mwitikio wa walipakodi ni mkubwa hapa Kasulu na mpaka sasa wafanyabiashara wengi wamefika hapa ofisini kwa ajili ya kupata huduma na elimu ya kodi na wengine tumewatembelea na bado tunaendelea kuwatembelea katika maduka yao," alisema.

Rose alisema wafanyabiashara wanaelimishwa kuhusu utunzaji wa kumbukumbu, matumizi sahihi ya mashine za EFD na kuhamasishwa kulipa kodi kwa hiari huku TRA ikipokea maoni na kushughulikia malalamiko yao.

Timu ya maofisa wa TRA kutoka Makao Makuu iko katika Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma ikiendelea na kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango.

# Mwigulu: Mtazamo huu utaua PPP

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema upo mtazamo hasi kwenye utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ambao unachangia kuiua.

Dk. Nchemba aliyasema hayo juzi bungeni jijini Dodoma wakati Bunge lilipoiidhinishia wizara hiyo makadirio ya matumizi ya Sh. trilioni 12.9 katika mwaka ujao wa fedha.

Alisema kamati imeshauri serikali kuhamasisha serikali za mitaa kuwa na mabadiliko na maandiko ya miradi ambayo ina sura ya kibiashara itekelezwe mfumo wa PPP.

"Siku hizi mbili au tatu tumekaa na benki zote tumewaeleza utaratibu huu unaopendekezwa na kamati, tumeshirikiana nao na tumegawanya miradi ambayo ni zaidi ya mradi 75 wameichukua na baadhi wamefikia hatua za juu, baada ya hapo watasema ipi wataitekeleza," alisema.

Waziri huyo alisema ushauri mwingine uliotolewa ni mtizamo hasi kuhusu miradi ya PPP ambayo ni kikwazo kwa serikali katika kuitekeleza na kuitaka itatuliwe.

"Suala la mtazamo hasi kwenye miradi ya PPP siyo jambo la serikali peke yake, hii ni mtazamo wa nchi nzima, ni mitazamo ya wananchi pia, suala hili linahitaji kupeana elimu ya kutosha," alisema.

Dk. Nchemba alisema wakati nchi inapata uhuru ni dhahiri serikali ingetekeleza miradi yote na wakati huo huo ikatoa huduma kwa jamii kwa sababu waliozihitaji walikuwa wachache lakini uhitaji wa kuitekeleza kwa kutumia PPP ulikuwa mkubwa zaidi ili nchi ijiekeleze katika majukumu ya kutoa huduma.

"Hili suala la mitazamo hasi linatakiwa lieleweke kwa Watanzania, kwa sasa Tanzania akitokea mwekezaji yupo na mtaji kamili na kutaka kuleta meli ya uvuvi kwenye kina kirefu cha Bahari wa Hindi na akitoka kwenye meli ajenge na bandari ya uvuvi, akitoka hapo aweke kiwanda cha kuchakata samaki.

"Kwa mtazamo wa Kitanzania tulio wengi swali la kwanza utasikia, huyu ana mtaji kweli? Siyo tapeli kweli? Wakijiridhisha siyo tapeli, swali la pili, hatatuibia kweli? Wakijiridhisha na akatokea mmoja akasema 'ninadhani wazo ni zuri, swali la tatu, huyu anayesema hivi hajala chochote?" alisema.

Waziri huyo alisema mlolongo wa maswali hayo matatu ndiyo unaoua PPP na kusisitiza ni lazima miradi itekelezwe kwa kuaminiana.

Alisema utaratibu wa PPP kwenye miradi inayoweza kuwa ya kibiashara ni jambo linatakiwa kuelimishwa na kuelewa na ni utaratibu unaoipa serikali kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Hata waandaaji wa miradi, bado lipo, hata serikalini lipo pia kukiwa na laini moja inayohusisha PPP na kukawa na laini nyingine inayotumia bajeti ya serikali itakayochangamkiwa ni ile ya bajeti ya serikali, hayo ndiyo mazoea hata kama itasuasua, hiyo ndiyo itapewa kipaumbele kikubwa," alisema.

Alioongeza kuwa serikali itaendelea kuwasisitizia wataalamu wao wafuate vigezo vinavyotakiwa kwa kufanya miradi ya mfano na kutoa elimu ili watu waone ni jambo linalowezekana.

Kuhusu misamaha ya kodi, alisema jambo hilo linaendelea kufanyiwa kazi na lipo hatua za mwisho na siku mbili zijazo (kuanzia juzi) watakuja nalo.

Akijibu hoja za baadhi ya wabunge waliotaka michango ya watumishi ipelekwe kwa wakati katika mifuko ya hifadhi ya jamii, Waziri Nchemba alisema wamepokea na majibu ya kudumu yatatolewa katika hotuba ya kesho ya Bajeti ya Serikali.

Kuhusu mapendekezo ya kamati kuwa serikali iache kutenga fedha fungu 21 linalohusu watumishi kwa ajili ya kupandisha madaraja, Dk. Mwigulu alisema utaratibu uliopo ni fedha hizo kutengwa kwenye mafungu husika na mwaka wa fedha 2021/22 zaidi ya Sh. bilioni 209 zimetengwa.



Baadhi ya wafanyakazi wa mgodi wa dhahabu wa Barrick wa Bulyanhulu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wakisafisha mazingira ya maeneo ya mgodi huo jana, kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani 2021. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabilioni yatumika uagizaji wa mbolea

**Na Beatrice Moses**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) imebainisha jinsi uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi unavyogharimu nchi mabilioni ya shilingi.

Kwa kutambua hilo, mamlaka hiyo imeona umuhimu wa kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea nchini.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alifafanua mipango yao kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyezuru kwenye ofisi zao siku tatu zilizopita na kuagiza suala hilo lifanyiwe kazi.

Dk. Ngailo alibainisha kuwa kwa mwaka jana pekee, zilitutumika zaidi ya dola za Marekani milioni mbili (Sh. bilioni 4.63) kuagiza mbolea nje ya nchi.

Alifafanua kuwa asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini huagizwa kutoka huko wakati asilimia 10 tu ndiyo inayozalishwa nchini.

"Fedha nyingi zinatumika kuagiza mbolea kutoka nje. Tukijaribu kuangalia kuanzia mwaka 2017 hadi 2020, kimetumika kiwango kikubwa cha fedha ambacho kinaweza kupunguzwa iwapo tutafanikiwa kuzalisha mbolea kwa wingi nchini," alisema Dk. Ngailo.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TFRA, Profesa Anthony Mshandete, alisema walipata nafasi ya kumjulisha waziri mambo kadhaa waliyokusudia kufanya ikiwamo juhudi za kuongeza ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja kupitia hatua ya mchujo wa awali kwa ajili ya kupata waagizaji wa mbolea nchini.

Profesa Mshandete alisema Waziri wa Kilimo ameagiza kufanya mambo kadhaa ikiwamo kuongeza muda wa kufungua zabuni kwa mwezi mmoja mpaka Julai 8 mwaka huu.

Awali ilipaswa kuishia Juni 18 mwaka huu lakini wamelazimika kuongeza muda kwa lengo la kupata washiriki wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi ili kuongeza ushindani.

"Tangazo la zabuni lipelekwe kwenye ofisi za balozi za Tanzania kwenye nchi zinazozalisha mbolea duniani kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa nia ya kupata washiriki. Mfano; Urusi, China, Saudi Arabia, Qatar, Morocco, Ukraine na Uturuki," alisema.

# Waitara afanya ukaguzi wa kushtukiza usiku

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, amesikitishwa na kusuasua kwa ujenzi wa daraja ya Kiyegea na kuagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Morogoro, kumpelekea taarifa ya ujenzi huo.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza usiku ya kukagua ujenzi huo ambao ulikuwa ukamilike mwezi Mei na kuiagiza TANROADS kumpelekea taarifa.

"Nimesikitishwa sana na ujenzi wa daraja hili sasa nimetoa agizo kwa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Morogoro kuniletea taarifa ofisini ikieleza ni lini ujenzi huu wa daraja la Kiyegea utakamilika kwani sioni sababu," alisema Waitara.

Alisema haoni sababu za msingi daraja hilo kushindwa kukamilika kwa wakati tangu liliposombwa na maji mwezi Februari mwaka 2020 na kumtaka mkandarasi anayejenga daraja kuongeza kasi zaidi.

Alisema Mkoa wa Morogoro kuna miradi mingi yenye malalamiko kutokana na kushindwa kukamilika kwa wakati ikiwamo barabara ya Kidatu-Ifakara nao kumtaka Meneja wa TANROADS kusimamia ujenzi huo ili kuepuka malalamiko.

"Ili kupepuka malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa mkoa huu ni wajibu wa TANROADS kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha barabara zote zinapitika bila kuwa na changamoto yoyote ile," alisema Waitara.

Aliitaka TANROADS mkoa huo kuhakikisha miradi yote wanayoisimamia inakamilika kwa wakati na kuwa mtumishi yeyote atakayeonyesha uzembe atamchukulia hatua.

Kwa upande wake Mhandisi Msimamizi wa mradi wa ujenzi wa daraja hilo la Kiyegea, Brown Kisamo, alisema kuwa ujenzi huo unakwenda vizuri na baada ya wiki moja kutakuwa na hatua kubwa imefikiwa.

Vile vile, alisema baadhi ya changamoto zinazokabili ujenzi huo zitatatuliwa na kumhakikishia Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuwa ujenzi huo mbali na kuchelewa, unafanyika vizuri.

Daraja la Kiyegea lililopo mpakani mwa Wilaya ya Kilosa na Gairo lilikatika mwanzoni mwa mwaka jana na wakati huo Rais Hayati Magufuli alifika eneo hilo na kujionea athari zilizopo na kutoa agizo kwa wizara husika.




Mbunge wa Liwale, mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka (kushoto), akikabidhi gari la wagonjwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Liwale, Luiza Mlelwa, kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kata ya Kibutuka, juzi. Gari hilo ni moja kati magari yaliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa baadhi ya halmashauri hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NTAP yakamata zaidi ya majangili 30,000

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

TAASISI za Uhifadhi kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kuzuia Ujangili (NTAP), kimewezesha kukamatwa wa majangili 33,386 na silaha 2,533 kipindi cha miaka mitano.

Kutokana na operesheni hizo jumla ya kesi 5,253 za watuhumiwa wa ujangili zimefunguliwa katika vituo mbalimbali nchini na 914 zimemalizika, watuhumiwa 1,600 wamefungwa kati ya miaka 10 hadi 30.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Ludovick Nduhiye, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya maofisa upelelezi na waendesha mashtaka ya makosa ya ujangili kwa watumishi wanaounda kikosi hicho kutoka vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama.

Mafunzo hayo makosa na misitu yanafanyika mjini Morogoro kwa muda wa siku nne kwaajili ya kutathmini kazi iliyofanywa na kikosi hicho cha kitaifa cha kupambana na ujangili.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema katika kipindi hicho kikosi kazi hicho kilikamata nyara mbalimbali zikiwamo meno ya tembo vipande 14,741, pembe za faru 25, wanyama hai aina ya kakakuona 10, kobe 962 na viumbe hai jamii ya mijusi 700.

Akielezea mafanikio ya kikosi hicho, alisema hali ya ujangili kwa sasa imepungua kwa asilimia 90, viashiria vinaonyesha kuwa vitendo vya ujangili vimepungua pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wanyama katika hifadhi mbalimbali.

Alisema pia mafanikio hayo yamewezesha watuhumiwa wanaokamatwa idadi yao imeendelea kupungua kutoka 547 mwaka 2016 hadi kufikia watumiwa 326 mwaka 2019 na 185 katika kipindi cha mwaka jana.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Dk. Maurus Msuha, alisema kutokana na kuanzishwa kwa kikosi na utekelezaji wake wa majukumu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, viashiria vinaonyesha idadi ya tembo inaongezeka kutoka 43,521 mwaka 2015 hadi kufikia tembo 60,000 mwaka 2020, pia kupungua ukamatwaji wa nyara nje ya nchi zinazotoka Tanzania tangu mwaka 2016 hadi 2020.

Alisema jukumu kubwa walilopewa ni kuimarisha ulinzi, uhifadhi wa maliasili, wanyamapori na misitu ili kukuza utalii hatua mbayo itasaidia kuongeza idadi ya watalii kutoka milioni 1.5 hadi kufikia milioni tano kwa mwaka kufikia 2025 na kuongeza mapato kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.6 kwa mwaka 2020 hadi Dola bilioni sita kwa mwaka 2025.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) Camilluis Wambura, alisema mafunzo hayo yameletwa kwa muda mwafaka kutokana na changamoto ya baadhi ya watendaji wa serikali wakiwamo wapelelezi na waendesha mashtaka kutofuata misingi ya utekelezaji wa majukumu yao na kusababisha baadhi ya kesi za ujangili kutopata mafanikio mahakamani.

Akimwakilisha Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Paulo Kadushi, alisema upelelezi wa makosa ya jinai hususani ya wanyamapori na misitu, alisema umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa pamoja na ushirikiano hafifu baina ya vyombo vya upelelezi.

Alisema kwa upande mwingine, kumekuwa na changamoto kwa ushirikiano hafifu kati ya wapelelezi na waendesha mashtaka katika hatua ya upelelezi.

Alisema ni pamoja na upelelezi kufanyika bila kuzingatia masuala mengine mtambuka ambayo ni muhimu ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kifedha, masuala ya rushwa, utafutaji na ukamataji wa mapema unaotokana na uhalifu, ukusanyaji wa ushahidi kutoka nje ya nchi kutozingatiwa kwa mambo ya kisheria na ushahidi kutopokelewa mahakamani.

## Hali duni, tamaa vyadaiwa chanzo ujauzito wanafunzi

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

BAADHI ya wazazi wa Wilaya ya Kisarawe wamesema hali duni ya maisha ni moja ya sababu watoto wa kike kupata mimba na kukatisha masomo yao.

Wakiongea na Nipashe, walisema watoto wa kike wanaingia kwenye vishawishi vinavyowasababisha kupata mimba kutokana na kukosa baadhi ya mahitaji wawapo shuleni.

Mwanahawa Chakupewa, mkazi wa Makurunge, Kata ya Kiluvya, alisema yeye ni mmoja wa waathirika wa tatizo la watoto kupata mimba wakiwa shule kutokana na kushindwa kuwapatia fedha wanapokwenda shule.

Mwanahawa alisema watoto wake wawili wa shule ya msingi na sekondari walikatisha masomo baada ya kupata mimba na alipofuatilia alibaini hali hiyo ilichangiwa na kukosa fedha ya kila siku kuwapatia watoto wake.

"Nilitengana na mume wangu tangu mwaka 2011 aliniacha na mabinti watatu wakiwa wanasoma, kazi yangu ni kilimo nalima vibarua ndio nipate chakula na matumizi mengine sikuwa na uwezo wa kuwapatia hata Sh. 500 kwa siku ili wanunue vitu wakiwa shule," alisema.

Alisema kuna wakati watoto wake walikua wakilalamika wenzao wanavyonunua vitu vya kula wakiwa shuleni huku wao wakibaki kuwaangalia, lakini kwakua hakuwa na namna alimudu kwa mara chache mara moja kwa mwezi kuwapatia kila mmoja Sh. 500.

"Na hiyo Sh. 500 walipata tu endapo nitabakisha baada ya kubakisha nikishanunua vyakula, zaidi ya hapo sikuwa na chakuwapa hadi wanaporudi kutoka shule wakute chakula ndio wanakula hii naona ndio sababu ya wao kuingia kwenye vishawishi," alisema. Alisema watoto wake walikatisha masomo mmoja akiwa darasa la tano na mwingine kidato cha kwanza.

Naye Asha Selemani, mkazi wa kitongoji cha Gama Kisarawe, alisema mjukuu wake alikatisha masomo akiwa kidato cha tatu baada ya kurubuniwa na vijana na kupata mimba.

Alisema licha ya kumpatia mahitaji yake pamoja na pesa ya kwenda shule, lakini tamaa ilimponza.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Makurunge, Joseph Kabogo, alikiri maisha duni kwa baadhi ya wazazi kuwa chanzo cha watoto wao kupata mimba wakiwa shuleni.

Kabogo pia alisema baadhi ya wazazi hawajajenga tabia ya kufuatilia watoto wao na kusababisha wanapobadilika tabia kutogundua mapema kabla ya kupata ujauzito.

Mmoja wa wanafunzi aliyehitimu Shule ya Sekondari ya Makurunge, Tatu Juma, alisema wanafunzi wengi hawaridhiki na maisha ya familia zao na kuingia kwenye vishawishi ili wapate fedha.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Kisarawe, Patrick Gwivaha, mwaka 2020 wanafunzi wa kike 39 wa sekondari walikatisha masomo baada ya kupata ujauzito.

# Alizeti kuwa kilimo cha mkataba

BUNGE limeelezwa kuwa kuanzia msimu wa kilimo wa 2021/22, kilimo cha alizeti kitakuwa cha mkataba ikiwa ni jitihada za kukabiliana na tatizo la mafuta ya kula nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kuimarisha kilimo cha mkataba kwa njia ya Outgrower Scheme ili kupanua wigo wa upatikanaji wa soko kwa wakulima wadogo wadogo.

Akijibu, Bashe kilimo cha mkataba kinawezesha wakulima kuwa na soko la uhakika na wanunuzi kununua mazao yenye ubora kulingana na mahitaji.

Aidha, alisema dhana ya kilimo cha mkataba ni kuchangia kutatua tatizo la upatikanaji wa pembejeo za kilimo na kuimarisha upatikanaji wa mitaji kutokana na makubaliano baina ya mkulima, Taasisi za fedha na wanunuzi wa mazao husika kulingana na mahitaji ya soko.

"Kuanzia msimu wa kilimo wa 2021/22 kilimo cha alizeti kitakuwa cha mkataba na mpaka sasa Wizara imewasiliana na wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ili kusimamia kilimo mkataba," alisema.

Alisema kilimo cha mkataba kimeleta matokeo mazuri katika zao la ngano katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Arusha.

"Aidha, kampuni ya Pyxus Agriculture Tanzania Limited, Mount Meru Millers Ltd, Mwenge Sunflower Oil Mills Company Limited na Jackma CO. Ltd yamefanya vizuri katika mikoa ya Manyara, Dodoma na Singida," alisema.

Alisema kwa kutumia kilimo cha mkataba Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kuhamasisha wakulima kushiriki katika kilimo cha mkataba, ambacho kimeonyesha mwelekeo mpya katika kuhakikisha masoko ya uhakika, bei nzuri na viwango bora vya mazao ya kilimo.

"Wizara inatekeleza haya kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na maelekezo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa sekta ya kilimo ijitegemee," alisema.



Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, akijibu baadhi ya maswali Bungeni Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Aomba ukarabati wa kituo cha polisi

SERIKALI imeombwa kukifanyia ukarabati na kukipanua kituo cha polisi cha Nanyamba kutokana na majengo yake kuwa chakavu ili kikidhi mahitaji ya sasa.

Ombi hilo lilitolewa bungeni jana na Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alipokuwa akiuliza swali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika swali lake, Chikota alisema kituo hicho ni cha muda mrefu na kilikuwa kwa ajili ya kuhudumia tarafa ya Nanyamba lakini kwasasa ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Nanyamba, hivyo kuwapo na ongezeko la watu.

"Kituo hicho kimechoka na kesho kutwa nitakabidhi bati 70 kwa ajili ya kukarabati, je, serikali ina mpango gani wa ukarabati mkubwa au kujenga kituo cha polisi Nanyamba?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamza Khamis Chilo, alimpongeza Mbunge huyo kwa juhudi za kutatua kero zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo.

"Zipo jitihada za serikali tutafanya si kituo hichi tu alichokitaja pia tunafanya kwa vituo vingine, tutaangalia na bajeti itakavyoruhusu na tumuahidi moja ya eneo tutakalowapa kipaumbele ni kuhakikisha wananchi wanapata kituo bora na kufanya ukarabati katika kituo hicho," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kiwani (CCM), Abdallah Rashid Rashid, alitaka kujua lini Serikali itajenga kituo cha polisi katika jimbo la kiwani ili kuepusha wananchi kufuata huduma za polisi masafa marefu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chilo, alisema serikali inatambua hitaji la kituo cha Polisi eneo la Kiwani na kwa sasa wananchi wa Kiwani wanapata huduma ya polisi kutoka katika kituo cha Polisi Kengeja ambacho kipo umbali wa kilometa tano kutoka Kiwani Centre eneo linaloitwa Mendes.

Alisema mpaka sasa sehemu ya Kiwani hakuna eneo lililotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwa ajili ya kujenga kituo cha Polisi na nyumba za makazi ya askari.

"Ni ushauri wangu kwa mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya pamoja na wananchi ili kutoa eneo kwa jeshi la polisi litakalotosha kwa mahitaji ya ujenzi wa Kituo cha Polisi pamoja na makazi ya askari, ili Jeshi la Polisi liweze kutoa huduma karibu na wananchi katika eneo la Kiwani," alisema.

# Serikali yatakiwa kudhibiti wizi wa vyuma

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis, ameitaka serikali kukabiliana na wizi wa vyuma unaosababishwa na kushamiri kwa biashara ya chuma chakavu.

Akiuliza swali, Mbunge huyo alihoji serikali haioni biashara ya vyuma chakavu ni hatarishi hata kwa usalama wa raia na mali zao.

Akijibu, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Hassan Chande, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, kupitia Vifungu vya 133 -139, Serikali imeweka kanuni za udhibiti wa taka hatarishi ikihusisha ukusanyaji, usafirishaji na uhifadhi wa taka hatarishi.

"Sambamba na uwepo wa kanuni, serikali imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali pamoja na elimu kwa jamii katika ulinzi wa miundombinu,"alisema.

Aidha, alisema serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na polisi imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda ili kudhibiti uhujumu wa miundombinu ya serikali na watu binafsi.

"Biashara ya vyuma chakavu imesaidia kuziondosha taka hizi katika mazingira na hivyo kutengeneza mazingira safi na salama kwa afya ya binadamu," alisema.

Aidha, alisema vyuma chakavu ni malighafi ya viwanda hasa viwanda vya nondo na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Hata hivyo, alisema serikali imekuwa ikifanya ufuatiliaji ili kudhibiti hujuma ya miundombinu ya Serikali na watu binafsi.

Aliwaomba wananchi na vyombo mbalimbali kushiriki pamoja katika kulinda miundombinu dhidi ya watu waovu na wasio wazalendo.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

# ama

ALHAMISI JUNI 10, 2021

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

KARNE TATU ZA KILIMO NGORO

## Tija mazao bila mmomonyoko milimani, rutuba na kupendezesha ardhi Mbinga



Ukurasa 12

SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

## Dk. Mpango: Suluhisho nishati mbadala

SIKU YA HEDHI

# ‘Wenye jambo lao’ wapigana kutafuta haki iliko, shinikizo iwamo katika bajeti

## ■Meya, Diwani watikisa kichwa ’ndiyo’

**Na Yasmine Protace**

INAWEZEKANA kudiriki kutamka hedhi salama sasa ni kampeni rasmi kitaifa, katika sura tofauti. Sura ya utetezi ikitoka pande nyingi za umma, ngome kuu ni kutoka kwa kinamama.

Muhimu katika hilo ni nini? Inatakiwa mtu azingatie, tena iwe kwa msichana au mwanamke, katika kuepuka maambukizi ya magonjwa.

Pamoja na kudai hedhi salama kwa wanawake na watoto shule, pia kumekuwapo shida kubwa kwa baadhi ya familia zinazoshindwa kumudu gharama za taulo za kike.

Uhalisia uliopo, ni kwamba hadi sasa kuna familia ambazo zina wakati mgumu kumudu namna ya kusimamia maisha yao kila siku, hata kuthubutu milo milo mitatu.

Hiyo, pia iko katika sura nyingine, mtihani mgumu katika harakati za kumudu kununua taulo za kike kwa mabinti au kinamama na haishangazi kuiwashuhudia mabinti na hasa shuleni, wanajistiri kwa vifaa visivyofaa.

**KUTOKA MAADHIMISHO**

Katika kusherehekea maadhimisho ya Siku ya Hedhi Duniani ,baadhi ya washiriki waliomba taulo za kike ziwe zinatolewa bure





Waziri Dk. Dorothy Gwajima; wizara yake ni muwajibikaji mkuu katika kutetea hedhi salama. **PICHA: MTANDAO.**

kama ziavyogaiwa mipira ya kiume, maarufu kondomu.

Bishagazi Delema, ni Mwenyekiti wa Kituo cha Maarifa na Taarifa, kilichopo Kipunguni jijini Dar es Salaam, anasema kuwa serikali inapaswa kufanya mpango wa kutoa bure taulo za kike kwa mabiniti, kama kondomu zinavyotokewa bure katika baadhi ya maeneo.

Anasema, katika baadhi ya ofisi kondomu zinawekwa mpaka vyooni kuhamamsisha kinga, katika kusherehekea baadhi ya maadhimisho, kila atakaye inakuwa ruksa kwake kuchukukua.

“Tukumbuke kuwa kuna watu waishio maisha magumu, hata milo mitatu kwa siku hawapaki, sasa watawezaje kumudu kununua taulo za kike,” anahoji.

Anaongeza kuwa wananchi wanapaswa kujenga utamaduni wa kushiriki mikutano ya kijiji, ili waweze kuizungumzia bajeti yenye mlengo wa kijinsia, itakayokuwa mkombozi kwa mwanamke.

**KIONGOZI MTANDAO**

Mwenyekiti wa Mtandao wa Vituo vya Maarifa na Taarifa Ubungo, Neema Mwinyi, anasema vituo vya taarifa na maarifa mkoa Dar es Salaam, vinavyofadhiliwa na asasi TGNP Mtandao, mtazamo wake ni kumkomboa msichana katika bajeti ya mlengo wa kijinsia.

Anasema shule nyingi zinakabiliwa na ukosefu wa maji ndani ya vyoo, ukosefu wa shimo la kuchoma taulo zilizotumika na ukosefu wa vyumba vya kujistiri.

Neema anasema Siku ya Hedhi ina manaa kwa mataifa kujenga uelewa na kupaza sauti katika jinsi ya kupata huduma nzuri za kusaidia wanawake kuwa salama, wanapokuwa kwenye hali hiyo.

Anasema ni ukweli ulio wazi kwamba hata matatizo mengi ya wanawake kuhusiana na uzazi, chimbuko lake ni kushindwa kwao kukabiliana na hedhi kwa njia salama, hasa wanapokuwa katika umri mdogo.

“Umoja wa Mataifa ulilipa uzito wa kipekee siku hiyo, baada ya kuona kwamba kwa nchi zinazoendelea, mwanamke akiwa katika hedhi anapata tabu zaidi kwa sababu vifaa vya kujistiri vina gharama kubwa sana na gharama za kuzimudu hawawezi,” anasema.

Pia, anafafanua kwamba wanapokuwa katika maadhimisho hayo, wao kama wadau huwa na utetezi katika usawa wa kijinsia na haki za wanawake wametoa ushauri wao.

Neema anashauri kwamba, jamii zivunje ukimya walio nao kwenye masuala yanayohusiana na hedhi salama na

familia zinapaswa kutoa kipaumbele, katika bajeti inatimiza yaliyo muhimu katika kuhakikisha nyumbani kunapatikana vifaa na nyenzo za kutisha.

Msisitizo wa mama huyo ni kwamba, mara zote hedhi ambayo kibaiolojia ni sehemu ya maisha ya mwanamke na kutokana na uhalisia huo, ni muhimu shule kuwa na mwalimu mlezi anayewasimia mabinti kuwapa ushauri.

Neema anaenda mbali kwamba, halmashauri zinapaswa kutenga bajeti ya kutosha ya kutoa pedi bure kwa mabinti shuleni, sambamba na kuboresha matundu ya vyoo.

**VIONGOZI HALMASHAURI**

Hoja ya Neema, inaungwa mkono na Diwani wa Viti Maalumu katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Kiberatha Samboni, anayesema hedhi salama ni jambo la lazima kwa kila mwanamke na msichana.

Anasema, katika halmasahuri wako katika hatua ya kuamua na itafika wakati watakaoamua, hata kuwa katikia nafasi nzuri ya kulizungumzia suala hilo, shinikizo lililopo ni katika mwaka ujao wa fedha kutengwe bajeti mahsusi.

Mama huyo diwani, anasema wanatamani taulo za kike zitolewe bure, nao kinamama kwa umoja

Endelea Uk. 13

MAZINGIRA

## SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

# DK. MPANGO: SULUHISHO NISHATI MBADALA

**Na Christina Mwakangale**

INAPOFIKA kila Juni 5 ya mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku ya mazingira iliyoanza kuadhimishwa mwaka 1972. Lengo ni kuelimisha umma masuala ya mazingira.

Wiki hii maadhimisho yalikuwa jijini Dodoma, ilikohudhuriwa na wadau wa mazingira, viongozi wa serikali na taasisi, kulikobainishwa matumizi ya nishati mbadala kunusuru mazingira.

Wakati kaulimbiu mwaka uliopo kimataifa "Tutumie nishati mbadala kurejesha ikolojia," asilimia 90 ya Watanzania ni matumiaji mkaa na matumizi ya mbadala wake inaongezeka asilimia mbili pekee kwa mwaka.

Utumiaji kuni na mkaa katika meneo mengi, ni zao la upatikanaji kwa bei nafuu, ikilinganishwa na nishati mbadala kama gesi inayotajwa kuwa ghali. Mathalan, mtungi mpya wenye gesi ujazo wa kilo sita unauzwa wastani kati ya Sh. 40,000 hadi 50,000, kulingana.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alipokuwa kiwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo mjini Dodoma, alisema siku hiyo inalenga kuikumbusha jamii na serikali wajibu wa kutunza mazingira.

"Mwaka huu siku hii ikiadhimishwa kimataifa duniani Pakistan, kaulimbiu duniani ni kurejesha mifumo ya uhusiano na kutegemeana kati ya viumbe hai na mazingira," anasema Dk. Mpango.

Pia, kuna kaulimbiu inayozitaka nchi wanachama kutambua mazingira yanayotegemewa na wanadamu na wanyama kupata chakula, hewa safi na uhai kwa jumla.

**MAKAMU WA RAIS**

Makamu Rais anasema, Tanzania bado kuna wastani asilimia 80 wanaotumia mkaa na kuni, akiwa na ufafanuzi: "Tathmini iliyofanyika kupitia utafiti wa mapato na matumizi binafsi ya kaya mwaka 2007 na mwaka 2011/12 na 2017/18 inaonyesha kwamba katika kila kaya 100 nchini, kaya 90 zinatumia mkaa na kuni kama nishati ya kupikia."

Anasema, utegemezi wa nishati hiyo unaongezeka kila siku ukisukumwa na ongezeko la watu katika shughuli za biashara, pia soko la mkaa kisiwani Comoro.

Pia, kiongozi huyo mwanazuoni wa uchumi, anasema asilimia 80 ya rasilimali misitu na mazingira yanaharibiwa na matumizi ya nyumbani, kwa ajili ya kuni na mkaa na hasa mijini, ikiwa ni wastani wa ekari 188 za kila mwaka, hali inayotoa shaka ya kutoweka miti haraka, kuibua ukame na mifumo ya ikolojia.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. **PICHA: MTANDAO**

"Dar es Salaam pekee inatumia gunia za mkaa 500,000 kwa mwaka mmoja sawa, na tani 45,000 na mita za ujazo 75,000 za miti," anaeleza.

Dk. Mpango anasema, nishati mbadala inayotumika ni mafuta ya taa, baiogesi, nishati jua na gesi ya kupikia chakula, jumla yao bado inatajwa kuongezeka kwa asilimia mbili.

Wito wa Makamu Rais ni wafanyabiashara wa nishati mbadala wakiwamo wauza gesi ya kupikia wabuni na kusaidia wananchi wa kipato kidogo wamudu magumu hayo.

"Tatizo lililopo mbele yetu ni namna gani ya kupunguza bei ya gesi na majiko. Bei ya majiko, ishuke, vyuo vyetu na watafiti wengine, watafiti ili kubaini kwanini bei ya nishati na vifaa vyake vinakuwa juu, nini kifanyike? Serikali na sekta binafsi hatuna budi kutekeleza namna bora ya matumizi nishati mbadala," anasema Dk. Mpango.

Dk. Mpango anashauri umma uzingatie kaulimbiu za kimataifa, wizara, taasisi, wakala na wadau wa maendeleo wa misitu na mazingira, wakibuni nishati mbadala ya kupunguza utumiaji kuni na mkaa.

"Wakati mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere utaongeza uzalishaji nishati ya umeme sababu utazalisha megawati 2500, ukikamilika tunatarajia kaya zinazotumia kuni na mkaa zitatumia umeme," anaahidi neema.

Dk Mpango anashauri elimu itolewe kwa jamii kutunza mazingira, huku akitaja athari za mabadiliko mazingira yanayochangia mafuriko, kina cha maji baharini au maziwa kupanda, magonjwa, ukame, njaa na mafuriko, yote magumu kwa nchi maskini kumudu.

"Tulipozaliwa dunia hii tuliikuta inapendeza, ustawi wa viumbe na mimea, inatupasa tukumbuke wajukuu wetu na wajukuu wao wakute mazingira bora nao wafurahie maisha,"anasema

**NASAHA ZA UNEP**

Mwakilishi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) Tanzania, Clara Makenya, anajitambulisha wao ni wadau wakubwa wa mazingira nchini na wataendelea kuunga mkono juhudi hizo.

Anaahidi UNEP itaendelea kuhamasisha utunzaji mazingira na tayari kuna mradi wa muongo mmoja unaolenga kurejesha mfumo wa ikolojia na kukabiliana na uchafuzi mazingira hususani, mifuko ya plastiki ambayo yamepigwa marufuku nchini.

**WADAU WANENA**

Mtaalamu kutoka Taasisi ya Kuendeleza Teknolojia na Huduma ya Nishati Endelevu (TaTEDO), Shima Sago, anasema utafiti walioufanywa umebaini muda unaotumika, upishi kwa jumla na nishati inayotumika na utamadini wa mapishi katika kila nyumba.

Anafafanua matokeo ya utafiti na sababu zake ilikuwa ni namna matumizi ya nishati na gharama. Hapo ilijumuisha nishati na chakula, vifaa vya kupika, mbinu za mapishi na idadi ya walaji.

"Utafiti ulilenga maswali haya: je, kupika kwa gesi au mkaa ni ghali ukilinganisha na kupika kwa umeme? Lakini inaonyesha kupika kwa umeme ni nafuu zaidi, hutumika uniti mbili iwapo kuna vifaa sanifu vya kupikia kama 'pressure cooker' na 'rice cooker', bei ya uniti mbili ni sawa na Sh. 730" anasema, akitaja wastani wa gharama ya kupika kwa umeme ni Sh. 21,900 kwa mwezi.

Anataja mtungi wa gesi unauzwa Sh. 45,000, na gunia la mkaa Sh. 50,000 hadi Sh. 80,000 kwa mwezi jijini Dar es Salaam, havitoshi kwa familia kubwa.

Ushauri wake ni kwamba, nishati umeme inapotumika, inapunguza uchafuzi mazingira, inaboresha afya, kupunguza gharama, pia usafi.

**KAMATI MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Uratibu kampeni ya Hifadhi Mazingira na Usafi nchini, Seif Ally Seif, anasema siku hiyo ni muhimu kutoa elimu, kutokana na kuwapo uchafuzi wa mazingira, pia kusababishwa ukame.

Anaeleza, mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na kuchafuliwa mazingira na kamati hiyo yenye wajumbe 19 inayojumuisha wadau mbalimbali, lengo lake ni kuhakikisha kila kaya, taasisi na mkoa, katika kuwashirikisha kuunga mkono kampeni hiyo.

"Tutashindanisha na kupata washindi wa kitaifa, kuwajengea utamaduni imara vijana kutunza mazingira kuanzia ngazi za shuleni, vyuo vikuu," anasema Seif, anayeshauri itolewe katika ngazi zote za jamii, kila wakati na yasiishie kwenye maadhimisho pekee.

Mwenyekiti wa Mabalozi wa kampeni hiyo, Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Musa Salum, anasisitiza ushirikiano katika uhakika wa kulinda mazingira.

**WAZIRI JAFO**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, anakumbusha Azimio la Umoja wa Mataifa, kwa maadhimisho ya kila Juni 5.

Anasema Tanzania imeadhimisha kwa namna tofauti mwaka huu na fursa kwa washiriki zaidi ya 100 kuonyesha fani mbalimbali za utunzaji mazingira, akikumbusha kaulimbiu 'Mazingira Yangu, Tanzania Yangu, Ninaipenda Daima.'



Miti iliyonawiri katika milima ya Usambara. **PICHA: MTANDAO**

MAZINGIRA

# EU yaja na suluhisho kwa mabadiliko tabianchi ndani ya Afrika Mashariki

## •Mkakati unaorejesha ongezeko la chakula

**Na Maulid Mmbaga**

KUNA shida ya tabianchi duniani. Hivi sasa Umoja wa Ulaya (EU) umeamua kuchukua hatua ya kubuni mikakati yenye miradi sita, kusaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Hapo inaendesha ufumbuzi katika utoaji elimu kwa wakazi kuhusu uendeshaji shughuli za kimaendeleo, kwa kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mradi wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Mazingira, Mathew Mpanda, ameiambia Nipashe hivi karibuni kwamba EU inashirikiana na nchi husika katika haja ya kuhamasisha kuhamia kwenye nishati mbadala.

Katika hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, kuzindua maonyesho ya mradi huo jijini Dar es Salaam, mkurugenzi huyo anasema EU itashirikiana na serikali na asasi za kiraia kuhamasisha kuhamia kwenye nishati mbadala.

Pia, anaeleza namna umoja huo utakavyohamasisha kilimo kinachozingatia tabianchi, usimamizi endelevu wa maliasili na ukuaji mdogo wa kaboni, kulingana na malengo yake katika maendeleo endelevu, wakipunguza udhaifu dhidi ya tabianchi na kuongeza ustahimilivu wa muda mrefu.

Anasema, mkakati huo unadhamiria kusaidia maendeleo na utekelezaji wa michango ya kitaifa kwa namna ya uwazi na shirikishi, ili kuimarisha kudhibiti madhara dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

"Mazingira na mabadiliko ya tabianchi hujenga ustahimilivu na fursa za kutengeneza ajira zenye manufaa kwa mazingira kwa ajili ya maendeleo ya uchumi na ukuaji endelevu.

"Pia, kuna changamoto ya matumizi ya mkaa hasa mijini na katika huu mradi, una zaidi ya Sh. bilioni 60 na tumetenga kiasi cha Sh.bilioni 30, ambazo zitatumika kwa ajili ya kusaidia sekta binafsi katika kuleta mbinu mbadala za kupunguza matumizi ya mkaa mjini," anafafanua.



Mandhari ya milima ya Usambara. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, anasisitiza namna fedha hizo zitakavyosaidia kuwezesha kitakachowekwa na sekta binafsi, hata kuwasaidia wanaotaka kuwekeza katika nyanja hiyo na rasilimali fedha ya kuwezesha jitihada hizo. Mapanda anabainisha mikakati hiyo inayotekelezwa kupitia mradi huo wenye lengo la kukabiliana na mabadiliko tabianchi na athari zake kitaifa.

### USALAMA LISHE

Anasema, mabadiliko ya tabianchi yanahusisha kuongezeka mafuriko, ukame na dhoruba ambayo kila mwaka inaunda asilimia 90 ya majanga yanayohusiana na tabianchi, hali inayoibua dhiki ya chakula na lishe kwa jamii husika.

"Pia, ikiwa idadi kubwa ya watu wenye njaa duniani wanakabiliwa na majanga ya tabianchi, utokomezaji njaa na uhakikishaji lishe bora, kunahitajika juhudi kubwa kuboresha uwezo wa wananchi kuandaa kujibu na kustahimili majanga," anasema.

Ni mradi unaokusudia kuboresha upatikanaji na utumiaji chakula bora kwa wanawake na watoto, kupitia mawasiliano ya kubadili tabia za jamii.

Anakumbusha kuwapo ajenda ya kuzalisha anuwai na usambazaji vyakula maalum vyenye virutubisho katika wilaya za Bahi na Chamwino, Dodoma, Ikungi na Singida Vijijini.

### USTAHIMILIVU VISIWANI

Anasema, mradi huo unaangaza kukuza visiwa vinavyokabiliana na mabadiliko ya tabianchi na unaongoza jamii za Kitanzania zilizo hatarini kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa kutoa suluhisho dhidi ya athari zilizopo.

Ni mradi unaotumia vijiji vya mazingira na unalenga kuongeza na kutofautisha mapato, kuimarisha ustahimilivu na kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa Mpanda, zipo jamii 26 zilizolengwa na mradi huo zilizoko ndani na karibu ya kisiwa Pemba, zikitegemea mfumo wa ikolojia pekee kujipatia riziki, jambo linaliozidi kutishiwa na mabadiliko ya tabianchi.

### UNAIJUA ECOBOMA?

Mkurugenzi Mtendaji Mpanda, anaeleza mfano wa tabianchi stahimilivu kwa wafugaji unaotumia mfumo kijiji cha mazingira kuongeza na kutofautisha mapato, kuimarisha ustahimilivu na kupunguza udhaifu unaoruhusu mabadiliko ya tabianchi.

"Zaidi ya kaya 2000 zilizolengwa kwenye mradi huu. Ziko katika Wilaya ya Arumeru na hutegemea mfumo wa ikolojia pekee katika kujipatia riziki, jambo ambalo wakati mwingine wanaweza kukwama na kushindwa kufanya shughuli zao za kila siku kutokana na mabadiliko tabianchi," anasema.

Mpanda anafafanua kuwa mradi utazisaidia kaya hizo kujua njia mbadala wa kuendesha shughuli zao.

### UPANUZI WA SOKO

Katika mkakati huo, inaelezwa upo uwezekano mkubwa wa nchi kuathirika na mabadiliko ya tabianchi, kutokana na idadi kubwa ya wakazi vijijini, kutegemea kilimo cha mvua ambacho ni mwathirika mkuu wa mabadiliko ya tabianchi.

Pia, kuna Mpango wa Maendeleo wa Kikanda, unaokusudia kuchangia ukuaji uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, uitwao MARKUP, unaolenga kusaidia kuongeza mauzo ya biashara ya kilimo na bidhaa za bustani nje ya nchi. Yote inatajwa kukuza muungano wa kanda na kufikia masoko ya Ulaya.

"MARKUP inawasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati katika nchi mbalimbali kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda, kulenga bidhaa maalum za kilimo kama vile parachichi, kakao, kahawa, viungo, chai na kilimo cha bustani," anafafanua.

### MAENEO MLIMANI

Mpanda anataja mbinu jumuishi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika milima ya Usambara na Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, inayolenga kupunguza uwezekano wa kuathirika na mabadiliko ya hali ya hewa.

Anasema, zimelengwa jamii nane zinazopatikana karibu na misitu ya juu ya baioanuai katika milima ya Usambara Mashariki na inategemea mfumo wa ikolojia pekee kwa ajili ya kujipatia riziki, jambo ambalo ni rahisi kuathiriwa na tabianchi.

### MPANGO WA AFRIKA

Mpanda anaitaja 'FISH4ACP' kuwa ni mpango wa Shirika la Mataifa ya Afrika, Caribbean na Pasifiki (OACPS) unaolenga kuunda minyororo ya thamani ya uvuvi na viumbe maji kuwa endelevu.

Pia, anasema unatarajiwa kutekelezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na washirika wengine, kwa ufadhili kutoka EU na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Shirika la Ujerumani (BMZ).

Ziwa Tanganyika linalopatikana katika nchi za Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Burundi na Zambia, ina mamilioni ya wakazi wanaoegemea akiba zake tajiri za bioanuwai za maji, kwa ajili ya chakula na mapato.

Mpanda anaeleza kwamba, sehemu kubwa ya kinachovuliwa, kinapatikana moja kwa moja sokoni au inakaushwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na baadhi hufikishwa katika masoko ya Afrika Mashariki.

# 'WENYE JAMBO LAO' WAPIGANA KUTAFUTA HAKI ILIKO, SHINIKIZO IWAMO KATIKA BAJETI

**Inatoka Uk. 11**

wao watajitahidi kushawishi zifutiwe kodi, ili raulo hizo ziuzwe kwa bei nafuu.

Anasema tatizo lililopo sasa ni kwamba taulo hizo za kinamama umuhimu wake bado hauchukuliwi kwa mapana, ikiwamo ngazi ya familia kutokana na baadhi ya wazazi hawaoni umuhimu mtoto wa kike kwenda shule pale anapokuwa katika hedhi.

Mtazamo wake ni kuwapo elimu kwa jamii itolewe ili umma uamke na kutambua kwamba kuna umuhimu wanafunzi wa jinsia zote wasaidiane kwa yale yanayolazimika.

Naibu Meya wa Manispaa ya Ubungo, Hassan Siraji, anawataka walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kujistiri, pale wanapokuwa kwenye hedhi.

Anaeleza kuzifahamu baadhi ya shule zenye changamoto ya matundu ya vyoo na maji, akiwa na ufafanuzi:" Hizo changamoto tutazimaliza kupitia fedha za bajeti zilizojengwa kwa ajili ya kutatua kero kwa watoto wa kike."

Naibu Meya anawataka walimu kuwapatia elimu ya hedhi watoto wa Jinsia zote ili waweze kujitambua.

MWANAFUNZI JE?

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Misigani (jina tunalo), anasema kila shule inatakiwa kuwapo na eneo mahususi kwa ajili ya kuchoma taulo za kike pale wanapozibadilisha. Pia, anaongeza haja ya baadhi ya shule zinapasa kuwa maji nje ya vyoo vyao, hilo likiwa ni changamoto pale mtu anapotaka kujisitiri, huwa anaangukia magumu.

Hoja yake anaianua kuwapo haja ya elimu ya hedhi itolewe kwa makundi yote, kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wa kiume huwadhihaki wasichana pale wanapoingia katika hali hiyo.

Anataja kingine, ni kwa baadhi ya wazazi wa kiume wanaposhindwa kuwahudumia watoto wa kike na kuona hilo ni jukumu la mwanamke na sio la baba.

"Wapo mabinti wanaishi na mzazi mmoja wa kiume, wanapokuwa katika hedhi ukiomba pesa unaambiwa hilo ni jukumu la mwanamke na sio la mwanamume," anasimulia.

Binti huyo pia anawageukia kinamama, baadhi kila siku hucheza vikoba wanakotoa michango, lakini ni wagumu kugharmia bajeti za taulo za kike kwa mabinti zao.

MAZINGIRA

## KARNE TATU ZA KILIMO NGORO

# Tija mazao bila mmomonyoko milimani, rutuba inapendezesha milima Mbinga

• Watalii safarini husimama kushangaa maajabu

**NA Gideon Mwakanosya, MBINGA**

UNAPOTAJA ngoro, ni aina ya kilimo kinachohifadhi mazingira kwa njia ya asili, kikiaminika kuanza kutumiwa na wakulima kabila la Wamatengo wilayani Mbinga, mkoa wa Ruvuma, zaidi ya miaka 300 iliyopita.

Ngoro inatajwa kuanzishwa na wazee maarufu wa kabila la Wamatengo waliotoka nchini Malawi katika karne ya 17. Historia inaonyesha ni vizazi zaidi ya 10, tangu kilimo cha Ngoro kilipoanzishwa Mbinga.

Elineus Ndunguru, Mbunge Mstaafu wa Mbinga, anataja dhumuni la kuanzishwa kilimo hicho ni kuudhibiti udongo ardhini, ambao kwa kawaida huondolewa na maji au upepo kutokana na mmomonyoko wa ardhi.

Kimsingi, ni sehemu ya ardhi iliyoshiba rutuba ya kufanyia kazi mimea istawi na hatimaye kutoa mavuno mengi na bora. Nduguru anafafanua:

"Tunajua kuwa udongo ulio chini ya tabaka la juu hauna rutuba ya kutosha ya kuwezesha mazao kustawi vizuri, kutoweka kwa udongo wa juu kutoka shambani au bustani kwa njia ya mmomonyoko ni hasara kubwa, kwa vile kunasababisha upungufu wa mavuno."

Mbunge huyo ambaye pia ni Mkurugenzi Mstaafu wa Wanyamapori nchini, anazitaja njia za kuhifadhi ardhi zinazoweza kutumiwa, inaendana na uhalisia wa hali ya hewa, miinuko, pia tambarare, zikibeba njia kuu mbinu za kienyeji na kisasa ambazo zimefanyia utafiti wa kina

### NASAHA ZA DARASANI

Hapo kuna maandiko kama ya wataaluma ambao kila mmoja anajulikana kwa jina moja, Bike katika mwaka 1938, Stenhouse mwaka 1994, pia Temu na Bisanda mwaka 1966, wanaoeleza jamii ya Wamatengo walilazimika kutumia kilimo ngoro kuhifadhi udongo mzuri kwenye miteremko ya milima yao.

Katika mashimo ya ngoro, yanapandwa mazao kama maharagwe, mahindi na ngano kwenye kingo za mashimo hayo na mkulima hufyeka shamba lake na kisha mkulima anazipanga kwenye mashimo ya ngoro.

Pia, mkulima huyo anawajibika kupindua udongo wa chini kwenda juu, anakata nyasi penye udongo wenye rutuba, anaugeuza kuwa mboji, hapo rutuba ikiongezeka.



Mbunge Mstaafu wa Mbinga, Ngwatura Ndunguru, akielezea mfumo wa kilimo cha ngoro, unaoendeshwa na jamii ya Wamatengo kwa namna tofauti. **PICHA: MTANDAO.**

Kitaalamu, maji ya mvua yanaposimama katika mashimo ya ngoro, yana kawaida kulinda unyevu ardhini yakikinga mmomonyoko wake na inaaminika ngoro inahusishwa na kuwapo mapango ya kuishi binadamu.

Hadi sasa, historia ya Mbinga inaonyesha kuwa zamani wananchi wa wilaya humo walikuwa na kilimo cha kuhama.

Staili yao ni kwamba, ngoro inaendeshwa sehemu moja na wanapogundua rutuba imeisha, wanahamia kwingineko kwenye rutuba na wanaendesha kilimo pasipo kujali athari za kimazingira zilijitokeza, kutokana na aina hiyo ya kilimo.

### ILIKOANZIA NGORO

Historia ya kilimo hicho ni kwamba, wazee wa kabila la Wamatengo waliamua kuanzisha kilimo cha kufukia majani, ili kupata mbolea ya asili. Hapo ndipo penye mwanzo wa kilimo cha ngoro.

Walimaji waliendelea pasipo kuhama, huku wakirutubisha ardhi na kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokana na ardhi ya Mbinga kuwa na milima yenye miteremko mikali.

Mbunge Mstaafu Ndunguru, anafafanua kuwa tangu jamii ya Wamatengo waanzishe kilimo ngoro miaka 300 iliyopita, hadi sasa wamekuwa na tija ya kuzalisha vyakula vingi na wanahifadhi mazingira kwa njia ya asili, wakizuia mmomonyoko wa udongo kutoka kwenye miteremko ya milima inayowazunguka.

Anasema kwamba wakati wanaendesha kilimo hicho cha ngoro, unapofika msimu wa mvua, maji huingia kwenye mimea na majani yaliyowekwa chini yanaoza.



Ndunguru anasema, inapofika hatua msimu mwingine, ni kawaida majani yanayoota kwenye mashimo yanafyekwa na mazao yaliyosalia yanavunwa na kutandazwa kwenye shimo, yanafukiwa tayari kuwa mboji.

Mzee John Mbunda, mwenye umri miaka 80, mkazi wa Kijiji cha Kilanga Juu wilayani Mbinga, anasema jamii ya Wamatengo walianzisha mfumo maalum wa kilimo Ngoro, zama za ujana wao walipoibatiza jina Ingoro.

Anasema, ni mfumo uliowawezesha kuendelea kulima kwenye maporomoko ya milima pasipo kusababisha mmomonyoko wa udongo au kuathiri vibaya rutuba mashambani.

Alex Ndunguru, mkazi wa kijiji cha Ilela, anasema wenyeji wa Mbinga walilazimika kubuni kilimo ngoro, ili kuhifadhi udongo kwenye miteremko ya milima Matengo na ukawa mkombozi kwa kuwa kilimo endelevu na mbadala wa mfumo wa zamani, Wamatengo walipokuwa wanaha.

### FAIDA MKAKATI

Utafiti umeonyesha kwamba, teknolojia imetoa majibu kwamba ngoro ni bora zaidi katika kilimo na wakulima wa maeneo mbalimbali wamekuwa wakifika wilayani Mbinga kujifunza namna inavyohifadhi ardhi na kutunza mazingira kwa muda mrefu.

Faida mojawapo, ni pale mvua zitanyesha na panaendelea kuwa na unyevu kutokana na maji yaliyomo kwenye shimo, huku Mbunge Mstaafu Ndunguru, anasema wameshaanza kutangaza kilimo na kukiingiza kuwa miongoni mwa vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Wilaya ya Mbinga pekee.

Baadhi ya wageni ambao wamekuwa wakitembea kwenye magari kupitia barabara ya Mbinga hadi Mbambabay Wilaya ya Nyasa na maeneo mengine ya milima ya Umatengo, wamelazimika kuisimama kila mara, kushangaa milima hiyo na kuchukua picha za kawaida na video.

Ndunguru anasisitiza, kilimo cha ngoro kina mvuto kwa wengi wa ndani na nje ya nchi, hasa katika mimea inayochomoza na kuonekana mfano wa mapambo katika milima ya Umatengo.

### MRADI WA WIZARA

Wizara ya Kilimo imeanzisha mradi wa Kufufua Mifumo Muhimu ya Asili ya Kilimo Duniani (Global Importance Agricutural Heritage System- GIAHS), ili kuendeleza Kilimo asili na kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji.

Taarifa ya Idara ya Matumizi Bora ya Ardhi wizarani, inaeleza mradi huo unatekelezwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ukilenga kutambua mifumo ya asili na endelevu ya kilimo na ufugaji, ili kumsaidia mkulima.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo katika Afrika Mashariki, Tanzania na Kenya zilichaguliwa kufufua mifumo hiyo kwa kuwa zina sehemu muhimu za kuendeshea na Tanzania ilipendekeza mifumo mitatu ya kilimo asili ukiwamo, mfumo wa ngoro.

Mifumo ya asili ya kilimo ilianza kupendekezwa duniani tangu mwaka 2002 na baadhi ya zinazotumia katika kilimo ni Japan, Ufilipino,China na Ujerumani.





# TFRA kuanza kutoa vibali kuuza mbolea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Mbolea Tanzania (TFRA) imeagizwa kuanza kutoa vibali vya kuuza mbolea iliyoingia nchini badala ya vibali hivyo kutolewa ofisi ya Waziri wa Kilimo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alitoa maelekezo hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Mbolea (YARA), jijini hapa.

Alisema ili kuongeza ufanisi zaidi wa utendaji vibali hivyo vitatolewa kwa njia ya mtandao na Ofisi ya Waziri wa Kilimo itakuwa na jukumu la kupewa taarifa ya utekelezaji wa utoaji vibali uliofanywa na TFRA.

Waziri Mkenda alisema kuwa serikali ina matumaini makubwa na wafanyabiashara wa mbolea kwa kuwa inaamini kuwa kurahisishwa utolewaji wa vibali hivyo kutawaongezea kasi ya kuagiza mbolea nyingi itakayoingia nchini kwa ajili ya matumizi ya wakulima wa ndani na nje ya nchi.

Kuhusu gharama za usafirishaji wa mbolea kupitia barabara, Prof. Mkenda alisema kuwa atafanya mazungumzo na Hazina ili kuona uwezekano wa huduma za kusafirisha mbolea kama itawezekana kutoa Ongezeko la Thamani (VAT).

"Tumegundua kuwa kusafirisha mbolea kwa reli kunapunguza sana gharama kwahiyo tumehimiza mbolea isafirishwe kwa reli kwenda Kaskazini kwa maana ya mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Manyara pamoja na kusafirishwa kwa reli kupitia njia ya kati mikoa ya Morogoro, Singida, Dodoma, Singida na Tazara tutafanya hivyo," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kupunguza gharama za mbolea nchini serikali imeielekeza TFRA kuhakikisha kuwa inaongeza muda wa zabuni ambao waliutoa.

Kuhusu Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Waziri Mkenda alisema kuwa katika makubaliano ya kikao kazi cha wizara atatafutwa mtaalamu elekezi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule ya Biashara kukaa kwa kipindi cha miezi sita na kuishauri serikali nini kifanyike ili kuifufua taasisi hiyo.

Naye, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, alisema kuwa Waziri wa Kilimo ameendelea kukutana na wadau wa mbolea nchini ili kuhakikishia kuwa wakulima wanaendelea kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula na biashara na ili kufikia hatua hiyo ni lazima kuongeza matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima.

Alisema nchi mbalimbali duniani zinaitegemea Bandari ya Dar es Salaam katika kusafirisha mbolea na vibali vya usafirishaji wa mbolea kutolewa moja kwa moja na TFRA.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, akifafanua jambo kwa viongozi wanawake kutoka vyama vya Siasa 14 vyenye usajili wa kudumu, waliotembelea Ofisi za Tume, eneo la Njedengwa, jijini Dodoma juzi, ili kujionea shughuli zinazofanywa na Tume hiyo. Ujumbe huo uliratibiwa na Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa nchini kewa lengo la kuwajengea ufahamu wadau wake. **PICHA: NEC**

# 'Wenye ulemavu wawekewe miundombinu rafiki'

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, amewataka wataalamu wa majengo kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Dk. Nkullo aliyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja kwa watumishi wa vituo vya afya na zahanati kutoka kata tano za wilaya hiyo kuhusu upatikanaji wa huduma jumuishi za afya kwa watu wenye ulemavu iliyofanyika Kongwa na mafunzo hayo yalifadhiliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Foundation for Civil Society.

Alisema majengo mengi yaliyojengwa miaka ya nyuma wilayani humo hayana miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu suala linaloonyesha kuna unyanyapaa na ubaguzi kwa upande wao.

"Hata hapa ofisini kwangu jengo hili naona lilisahaulika, wataalam hawakuweka miundombinu rafiki ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kuingia kwa urahisi hapa, cha kusikitisha hata huko kwenye vyoo havipo vinavyoweza kutumia na ndugu zetu hao huu ni unyanyapaa na tena ni ubaguzi," alisema.

Aliwataka wahudumu wa afya kuonyesha upendo kwa vitendo kwa watu wenye ulemavu wanapo wahudumia kulingana na aina ya ulemavu badala ya kuwanyanyapaa na kuwabagua.

Kwa upande wake, Katibu wa Mkoa wa Dodoma Shirikisho la Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Justust Ng'wantalima, alisema kuwa unyanyapaa na ubaguzi bado unawakatisha tamaa wanapougua na kushindwa kupata huduma ya kiafya.

"Pamoja na sababu zingine za kiuchumi, kitaasisi na kijamii zinazowakabila watu wenye ulemavu, unawakatisha tamaa na kufikia hatua ya kuficha hali zao pale wanapougua na kufikia hatua ya kuacha kutafuta matibabu," alisema.

Aliviomba vituo vya afya na zahanati kuhakikisha wahudumu wanatoa huduma kwa weledi kulingana na ulemavu alionao mtu.

Naye, Mtabibu wa Afya Zahanati ya Mautya Kongwa, Suzana Petro, aliomba serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wahudumu wa afya na zahanati vilivyopo vijijini ili kuwahudumia ipasavyo kulingana na ulemavu alionao.

Alisema elimu hiyo pia itawawezesha wahudumu wengi kuwahudumia hata kwa njia za lugha ya alama ambayo imekuwa tatizo kwa upande wao.

# Wajasiriamali waomba kuwezeshwa mitaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJASIRIAMALI nchini wameiomba serikali kuwawezesha kupata mitaji itakayowasaidia kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko la bidhaa na kutoa ushindaji wa kibiashara kwa wazalishaji wa nje ya nchi.

Mwenyekiti wa kikundi cha wajasiriamali cha Tusumuke jijini Dodoma, Chritopher Dioniz, alisema hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema suala la mitaji kwa wajasiriamali nchini bado ni kikwazo kikubwa kufikia katika malengo yao ya kibiashara.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa hivi sasa wana soko kubwa la bidhaa wanazozitengeneza, lakini kikwazo ni idadi ndogo ambayo haikidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

"Tunaomba serikali yetu tukufu itushike mkono ili tupate mitaji ambayo itatuwezesha kuzalisha kwa kiwango kikubwa bidhaa zetu ili kukidhi mahitaji ya soko lililopo hivi sasa," alisema Dioniz.

Alisema serikali inatakiwa kuvitumia vikundi vya wajasiriamali na kuviwezesha kutengeneza umoja ambao utasaidia kuwa na bidhaa za kutosha katika soko.

"Sisi hapa tunauza vifaranga vya kuku wakati mwingine unapata oda ya mteja, lakini unakua huna vifaranga wa kutosha kama vikundi vitatengeneza mnyororo wa kushirikina kwa pamoja kila kikundi kitakuwa na jukumu la kuzalisha bidhaa kwa mujibu wa mahitaji ya soko," alisema.

Naye, Mariam Said, msindikaji wa bidhaa za vyakula jijini Dodoma, alisema kuwa wanakabiliwa na tatizo la vifungashio pamoja na kulifikia soko la nje.

Alisema hivi sasa wasindikaji wa bidhaa za vyakula nchini wanatumia vifungashio kutoka nje ya nchi kutokana kukosekana vyenye ubora nchini.

"Hivi sasa vifungashio tunachukua nchini Kenya ambavyo ndivyo vyenye ubora ukilinganisha na vya hapa kwetu," alisema.

Alisema kutokana na tatizo la ugonjwa wa corona kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa vifungashio kutokana na mipaka mingi kufungwa.

"Tunaomba serikali yetu kulifanyia kazi suala hili ili kupata wawekezaji wengi watakao wekeza katika viwanda vya utengenezaji wa vifungashio vyenye ubora vitakavyo wezesha bidhaa zetu kuingia katika ushindani wa soko la dunia," alisema.

**Alisema serikali inatakiwa kuvitumia vikundi vya wajasiriamali na kuviwezesha kutengeneza umoja ambao utasaidia kuwa na bidhaa za kutosha katika soko.**



# Mabasi 15 yazuiwa kusafirisha abiria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, imeyazuia mabasi 12 yanayofanya safari kati ya Mbeya na mikoa mingine kuendelea na safari kutokana na ubovu, hivyo kuhatarisha maisha ya abiria.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, aliongoza opereshani ya kuzuia mabasi hayo jana asubuhi alipofanya ziara ya kushtukiza katika kituo kikuu cha mabasi cha jijini hapa.

SACP Mutafungwa alifanya ziara hiyo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, la kuyakagua mabasi yote ili kuzuia ajali ambazo zinazuilika.

Kamanda Mutafungwa akiwa na maofisa mbalimbali wa polisi mkoa wa Mbeya, waliyakagua mabasi yote ya mikoani na kubaini mabasi hayo yakiwa mabovu kupindukia, hali iliyowafanya kutoa namba na kuwaamuru madereva wakayarekebishe.

Aidha mabasi mengine matano yalibainika kuwa na ubovu wa kawaida, hivyo madereva wakatakiwa kuyarekebisha kabla ya kuendelea na safasi.

Hatua hiyo ilisababisha mabasi 15 pekee yalibainika kutokuwa na ubovu wa aina yoyote kuendelea na safari.

Kamanda Mutafungwa aliwataka madereva wa mabasi hayo kuhakikisha wanayafanyia matengenezo kisha kuyapeleka kwa maofisa wa ukaguzi wa jeshi hilo kabla ya kuingia barabarani.

"Ole wao madereva wa mabasi haya ambao watapita vichochoroni wakayaingiza barabarani. Tutashughulika nao kwa nguvu zote. Wakishayatengeneza watayaleta yakaguliwe tena na ikibainika bado mabovu yatazuiwa tena," alisema Kamanda Mutafungwa.

Pia alisema jeshi hilo litaendelea kuwafuatilia madereva barabarani ili kuhakikisha wanatii sheri bila shurti huku akiwataka kuepuka kuingia kwenye mikono ya sheria.

Aliwataka madereva hao kuacha kuyapita magari mengine kwenye maeneo ambayo ni hatarishi kwa maelezo kuwa utaratibu huo ndio umekuwa chanzo cha ajali nyingi ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

Kadhalika, hivyo aliwatahadharisha madereva ambao wamekuwa wakicheza na mifumo ya kudhibiti mwendo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria kwa maelezo kuwa baadhi ya madereva wamekuwa wakicheze mifumo hiyo kwa makusudi ili wasionekane wanapovunja sheria. Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, alisema ukaguzi wa mabasi hayo utakuwa endelevu ili kuhakikisha wananchi wanasafiri bila kupata matatizo njiani.

Aliwataka madereva na wamiliki wa mabasi kuyafanyia ukaguzi wa mara kwa mara ili wakibaini kuwa ni mabovu, wayarekebishe mapema kabla hayajazuiwa kuingia barabarani.

"Hili ni tatizo maana mabasi yanayotoka hapa Mbeya kwenda mikoani yako 32 lakini ni mabasi 15 pekee ndiyo yameonekana yako vizuri. Hii ni hatari sana, tunawaomba hata abiria watuelewe maana lengo letu si kuwazuia kusafiri ila tunataka wasafiri wakiwa salama," alisema Kamanda Matei.

Juzi, IGP Sirro aliagiza mabasi yote nchini kufanyiwa ukaguzi ili kupunguza matukio ya ajali za barabarani.



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilbroad Mutafungwa (haonekani kwenye picha), pamoja na askari wakizungumza na baadhi ya abiria waliokuwa wamekata tiketi kwenye mabasi yaliyozuiliwa kutokana na ubovu, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## RAS amkabidhi ofisi mrithiwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ALIYEKUWA Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, amemkabidhi ofisi Katibu Tawala mpya, Dk. Angelina Lutambi, huku akiwashukuru wananchi na viongozi kwa ushirikiano waliompatia katika kipindi chote alichofanya kazi mkoani hapa.

Mtunguja alisema jana kuwa katika kipindi chote ambacho amehudumu katika mkoa huo ameshuhudia ushirikiano mkubwa wa watendaji kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka ngazi za chini.

Alisema hakuna kudharauliana kati ya sekretarieti ya mkoa na watumishi wengine hali ambayo imesababisha mkoa kupata maendeleo ya haraka.

"Hawa watumishi wana ushirikiano mzuri sana. Kwa kipindi chote nilichokuwapo hapa nimepata ushirikiano mkubwa, sasa nawaomba mwendelee kumpatia ushirikiano Katibu Tawala mpya kama mlivyokuwa mnashirikiana na mimi," alisema Mtunguja.

Alisema mkoa huo umepiga hatua kubwa za kimaendeleo ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ya afya, maji, barabara, elimu na miundombinu mingine.

Kwa upande wake, Dk. Lutambi aliwataka watumishi wote wa halmashauri na wakuu wa idara zote kuwa wabunifu katika kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wananchi.

Alimshukuru Mtunguja kwa kuwaunganisha vizuri watumishi wa mkoa huku akiahidi kuendeleza ushirikiano huo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

"Kitakachotusaidia zaidi ni kuwa wabunifu, huu ushirikiano uliokuwepo tutauendeleza na ikiwezekana tuongeze zaidi ili tuwahudumie wananchi vizuri," alisema Dk. Lutambi.

Mtunguja ambaye amehudumu kama Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya kwa takriban miaka tisa amehamishiwa katika Mkoa wa Morogoro.

# Mbeya yaweka mpango kumaliza upungufu wa mafuta ya kupikia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeanza mikakati ya kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kupikia kwa kuwaagiza maofisa kilimo wa ngazi zote kuanzisha mashamba darasa ya kuwafundishia kilimo bora cha alizeti na mazao mengine ya mbegu za mafuta.

Pia imewaagiza maofisa umwagiliaji wa halmashauri zote za mkoa kuanzisha skimu zote za umwagiliaji katika mkoa huo ili ambazo zina matatizo ziboreshwe na ikiwezekana baadhi yake zitumike kwa ajili ya umwagiliaji wa alizeti.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa, agizo hilo juzi alipokuwa anafungua kikao cha wadau wa kilimo wa mkoa kilichokuwa kimelenga kujadili Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020.

Alisema ofisa yeyote ambaye hataandaa shamba darasa atachukuliwa hatua kwa maelezo kuwa wanalipwa mishahara na kupewa vitendea kazi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na si kufanyia kazi binafsi.

Homera alisema kwa sasa nchi iko kwenye kipindi kigumu cha uhaba wa mafuta hali iliyosababisha bei ya bidhaa hiyo kupaa kuliko kawaida, hivyo ili kukabiliana na hali hiyo, zinahitajika juhudi za makusudi kwa wadau wote kushiriki.

"Lakini pia nitahitaji kila ofisa kilimo atuletee taarifa inayoonyesha idadi ya wakulima aliowafundisha kilimo bora na atueleze amewafundisha kulima zao gani. Haiwezekani unadai upewe mpaka pikipiki lakini kazi unayofanya haionekani," alisema Homera.

Pia aliwataka maofisa hao kuendelea kutoa elimu ya kilimo bora cha mazao mbalimbali kwa wakulima ili kuhakikisha tija inaongezeka na kuufanya mkoa uwe na usalama wa chakula na kukabiliana na udumavu.

Akiwasilisha taarifa ya mpango huo, Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema alizeti ni moja ya mazao ambayo yamewekewa mkakati maalumu wa kuyaendeleza katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema wastani wa uzalishaji wa alizeti katika mkoa huo ni tani 26,756 kwa mwaka na kwamba katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 mpaka sasa, uzalishaji umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali.

Madito alisema mkoa huo una maeneo mengi ambayo yanafaa kwa kilimo cha alizeti lakini uzalishaji na usindikaji uko chini kutokana na wakulima wengi kutozingatia kilimo biashara na kupambana na visumbufu vya mimea.

"Lakini tatizo lingine ni matumizi hafifu ya pembejeo, matumizi ya mbegu za kienyeji na matumizi ya mbinu duni za uandaaji na usindikaji wa mafuta. Serikali imeendelea kuchukua hatua kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo," alisema Madito.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi aliwataka wadau wa kilimo katika mkoa huo kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija ili kujiinua kiuchumi.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa yenye hali nzuri ya hewa inayoruhusu mazao mbalimbali kustawi, hivyo akawataka wadau kushirikiana na serikali kuwasaidia wananchi.

Bei ya mafuta ya kupikia katika Mkoa wa Mbeya kwa sasa ni kati ya Sh. 25,000 na 30,000 kwa lita tano huku dumu lita moja ikiuzwa kati ya Sh. 5,000 na 6,000.



# SMZ yajipanga malipo kwa mtandao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohammed Mussa, amesema Serikali ya Zanzibar iko mstari wa mbele katika kuhimiza taasisi mbalimbali kufanya malipo ya fedha kwa njia ya mtandao.

Amesema kulipia huduma kwa njia ya mtandao inapunguza mianya ya upotevu wa fedha na wizi kwa wafanyakazi wasiokuwa waaminifu.

Waziri Lela alisema hayo juzi mjini Zanzibar wakati akifungua mkutano wa malipo kwa njia ya mtandao kwa wadau na mawakala wa benki ya Equity.

Alisema hivi sasa dunia inapiga hatua za maendeleo, hivyo wakati umefika kwa Tanzania na Zanzibar kuendana na mabadiliko hayo.

Alisema Zanzibar inakuza uchumi wake kupitia sekta ya utalii, hivyo kuwapo kwa mfumo wa kifedha kwa njia ya kieletroniki kutasaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya utalii.

Waziri huyo alisema mwaka jana mapato ya serikali kwa asilimia 82 yalitokana na utalii, hivyo benki hiyo ina wajibu wa kudumisha mfumo wa kieletroniki ili kuwapa nafasi wageni wanoingia Zanzibar kupata miamala ya kifedha kwa urahisi.

"Niuombe uongozi wa benki hii kuhakikisha mawakala wenu wanapatiwa elimu. Ni lazima kufanya kazi kwa vitendo ya kuwasaidia wanajamii ili kuhakikisha amana zao zinakuwa salama wakati wote," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Equity, Robert Kibuti, alisema benki hiyo imejipanga kuhakikisha inawafikia wateja wake wote na kuwapa elimu ya mfumo wa malipo kwa mtandao.

Alisema katika kuhakikisha kuwa taasisi hiyo inawajali wananchi wake, hivi sasa huduma za benki hiyo zinapatikana katika maeneo mbalimbali ya Tanzania na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Kabuti, mfumo wa malipo kwa mtandao utarahisisha zaidi kwa wananchi ambao jamaa zao wako katika mataifa mbalimbali nje ya nchi kutumia huduma za kifedha.

"Tuna mpango wa kupanua wigo zaidi ili kuhakikisha wananchi na watalii wanaokuja Zanzibar wasipate usumbufu wa aina yoyote," alisema.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, Mkuu wa Mifumo ya Malipo wa Benki hiyo, Ralph Ligallama, alisema mfumo huo ni mzuri hasa kwa Zanzibar kwa vile watalii wengi wanaingia na utawarahisishia kuchukua fedha katika mabegi yao.

Naye wakala wa benki hiyo, Haroub Sudi, alisema mfumo huo si mbaya ila utachukua muda kuzoeleka na kuhakikisha mitandao inafanya kazi muda wote ila kuepusha usumbufu kwa wateja.



Katibu wa Umoja wa Dini Mbalimbali Zanzibar, Askofu Dickson Kaganga, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kumaliza mazungumzo na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), katika Ikulu ya Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Waziri ataja chanzo kudorora ufugaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kwamba sekta ya mifugo ikiwamo ng'ombe na mbuzi imeyumba kwa kiasi kikubwa na kutaja sababu za kukosekana maeneo ya kutosha ya malisho ya wanyama hao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said.

Katika swali hilo, Machano alitaka kujua mikakati ya serikali katika kuimarisha sekta ya mifugo na kuzalisha maziwa.

Alisema sababu zilizofanya kuyumba kwa sekta hiyo ni kukosekana kwa maeneo ya malisho ya mifugo kutokana na maeneo mengi sasa kutumika kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kudumu.

Waziri alitaja sababu nyingine kuwa ni ukosefu wa mbegu bora kwa wafugaji wa ng'ombe wa kisasa ambao ni maarufu kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa.

Pia alisema wizi wa mifugo ni miongoni mwa changamoto iliyojitokeza hivi karibuni hatua ambayo imesababisha wafugaji wengi kuanza kukata tamaa na maendeleo ya sekta hiyo.

Aliyataja maeneo ya Wilaya ya Magharibi A Unguja, ambayo awali yalikuwa yakitumika kwa ajili ya malisho ya wanyama kuwa hivi sasa yamegeuzwa kwa ajili ya matumizi ya makazi ya kudumu.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba ni kweli sekta ya ufugaji hivi sasa imeyumba sana kutokana na maeneo mengi ya malisho kutumika kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kudumu"alisema.

Aliitaja mikakati ya baadaye ya serikali kuwa ni kujenga kiwanda cha malisho ya chakula cha mifugo ambacho kwa kiasi kikubwa kitaimarisha sekta ya ufugaji.

# Mali 179 zaingizwa daftari la serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MALI 179,000 za serikali zimeorodheshwa na kuingizwa katika daftari la mali za serikali baada ya kuhakikiwa na kutambuliwa rasmi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za wajumbe kuhusu makadirio mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Waziri huyo alisema serikali imechelewa kufanya uhakiki wa mali zake kwa ajili ya kuzitambua na kuziingiza katika daftari na matokeo yake baadhi ya mali zimepotea.

Alisema mali hizo zimeingizwa katika daftari la kudumu la kielektroniki hatua ambayo sasa itaiwezesha serikali kuzifahamu kokote zilipo na kuziba mianya ya upotevu.

Pia alisema wizara inakusudia kuwasilisha mswada wa sheria katika Baraza la Wawakilishi ambao utaunda chombo chenye mamlaka ya kutambua mali zote za serikali kwa mujibu wa sheria.

Alizitaja mali zitakazohakikiwa na kuingizwa katika daftari za mali za serikali kuwa ni pamoja na nyumba za serikali, mashamba na viwanja.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya wizara hiyo, walionyesha kusikitishwa na serikali kushindwa kuanzisha daftari la kuhakiki mali ambalo kwa zaidi ya miaka mitatu nyuma limetajwa kuanzishwa kwake.

Mwakilishi wa Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema wako watendaji ambao wamekuwa wakijilimbikizia mali za serikali huku baadhi ya maeneo ya viwanja yakichukuliwa na watu kuuziana kwa sababu havijahakikiwa na kuingizwa katika daftari hilo ili kutambuliwa kwa mujibu wa sheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**REHEMA MAHARAGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 413 CUT** AINA YA TOYOTA LANDCRUISER YENYE CHASSIS NO **TRJ 150001B532**, ENGINE NO. **2TR1054597.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/ TR /RB/ 230/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BENEDICT ELIAS MBONDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya HONDA yenye namba za usajili **MC 786 CAZ** Chassis **No.5202764, Engine No.JH2PE06A17K20018 1.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/289925/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HASSAN ABDU DONASIAN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 986 BXG.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KAH/ TR /RB/ 302/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**KAPS LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki mbili aina ya **SKY MARC** yenye namba za usajili **MC 461 BHP** chasis namba **EOSC14X01009** engine namba B21,na kadi ya pikipiki aina ya **SKY MARC** namba za usajili **MC 870 AWE** chasisi namba **E0SC114X0112** engine namba **B21**,yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisis Polisi taarifa **DAR/OST/R-B/286336/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISAYA JACOB SAWE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya TOYO aina ya boxer yenye namba ya usajili **MC 453 AUQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/R-B/290505/2021.**

**AJ RECOVERIES LTD**
Your vision our future

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK(T)LIMITED**–,tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara nyumba ya mdaiwa sugu wa **LETSHEGO BANK TAWI LA MANZESE**, kama inavyoonekana hapa chini,

| S/NO | JINA LA MDAIW | DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU ,TAREHE,MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | VALENCY CHARLES KALANGA | NYUMBA (Plot no.726,Block "C",Madale,Manispaa ya Kinondoni.) | Mtaa - Madale Kata - Wazo Eneo - Mitikini | Siku -Ijumaa Tarehe -25/06/2021 Muda-Kuanzia saa 3 Asubuhi. |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipia sio chini ya asilimia 25% ya bei ambayo imefikiwa siku ya mnada na kiasi kilicho baki anataki wa kumaliza ndani ya siku kuminanne(14),endapo atashindwa kumalizia salio lililobaki mnada utarudiwa upya na fedha iliyolipwa haitarudishwa.Ukaguziwa dhamana ni kwa kuwasiliana na dalali au Tawi la benki Husika siku yoyote muda wa kazi.
2. Gharama za kubadilisha umiliki wa dhamana ni ya Mnunuzi.
3. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo.

**MAWASILIANO ZAIDI** AJ RECOVERIES LIMITED 0655 349937 / 0788 214 220

**OFISI ZA MATANGAZO**
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**

**KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**RUFAA NA: 63 / 2020.**

**ANECTUS JULIUS ......................MRUFANIWA**

**DHIDI YA**

**CELINA KAGYA .........................MJIBU RUFAA**

**KWA C ELINA KAGYA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa / unaarifiwa kuwa Rufaa Na. 63 / 2020 yamepangwa kutajwa tarehe 14.06.2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2: 00 asubuhi.

Hivyo unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe / mwakilishi wako mbele ya Baraza siku huyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa BARAZA hii leo tarehe 22.04.2021.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 27 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late FIDES JOSEPH MKWAWA of Miganga Mkonze within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JOSEPH.A. MKWAWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 9th Day of JULY 2021.

Dated at Dodoma this 4TH day of JUNE 2021

RESIDENT MAGISTRATE

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Jino la Patrice Lumumba kurudi DRC

**Kinshasa,** DRC

JINO la Patrice Lumumba, mtetezi wa Uhuru wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na mpambanaji dhidi ya ukoloni aliyeuawa mwezi Januari 1961, kabla ya mwili wake kumwagiwa tindikali, linatarajiwa kurudishwa Juni 21, mwaka huu.

Jino hilo la lilipatikana miaka mitano iliyopita kwa binti ya ofisa wa polisi wa Ubelgiji, aliyehusika wakati huo na kutoweka kwa mwili wa shujaa huyo.

Zoezi hilo litafanyika Juni 21, kabla ya mabaki ya waziri mkuu wa zamani wa DRC kuanza safari kwenda DRC hadi Juni 30.

"Kutakuwa na makabidhiano kwa familia na mara tu, mahali hapo, Ikulu ya Egmont (Brussels), kutakuwa na makabidhiano rasmi na mamlaka ya Ubelgiji na mamlaka ya DRC.

Rais Félix Antoine Tshisekedi Tshilombo atakuwepo kwa sherehe hii", alisema Balfu Bakupa Kanyinda, mtengenezaji wa filamu kutoka Ubelgiji mwenye asili ya Congo, aliyepewa jukumu na mamlaka ya DRC kuratibu sherehe hizi.

"Mnamo Juni 23, mwaka huu, mabaki ya Patrice Lumumba yatawasili kwenye ardhi yake ya asili huko Onalua ambako alizaliwa.

Onalua ilipewa jina la Lumumba-ville miaka miwili iliyopita, kutakuwa na maombolezo ya ukoo, maombolezo ya familia yake.

Asubuhi ya tarehe 25, mwili wa Patrice Lumumba utasafirishwa katika ngome yake ya kisiasa, mjini Kisangani, na tarehe 26, utafikishwa Lubumbashi, alipouawa.

Tarehe 27, mwili wa shujaa huyo utasafirishwa mjini Kinshasa, wakazi wa mji huo watatoa heshima zao kwa kiongozi huyo.

Na Juni 30, atazikwa mahali paitwapo Échangeur de Limete, "alisema Balfu Bakupa Kanyinda.

Mfalme Philippe wa Ubelgiji hatasafiri kwenda Kinshasa Juni 30 kwa mazishi ya kitaifa ya Patrice Lumumba kwa sababu ya mgogoro wa kiafya.

**RFI**

## Aliyempiga kofi Macron mkufunzi sanaa ya vita

**Drome,** UFARANSA

MTU aliyempiga kofi, Rais Emmanuel Macron huko Drome Ufaransa agundulika kuwa mkufunzi wa Sanaa ya Vita.

Vyombo vya habari Ufaransa, viliandika kwamba mshambuliaji huyo alikuwa akifanya Kendo ambayo ni sanaa ya upanga ya Mashariki ya Mbali, na kwamba alikuwa mkufunzi wa HEMA.

Ilielezwa kuwa mshambuliaji huyo alifuata akaunti za chama cha upande wa kulia kwenye mitandao ya kijamii.

Ofisi ya mwendesha mashtaka wa Valence, ilitangaza kuwa mshambuliaji huyo wa miaka 28, ambaye jina lake lilitambuliwa kama Damien T., na rafiki yake, ambaye alikuwa kizuizini naye, hawakuwa na rekodi ya jinai.

Wakati mshambuliaji huyo alipompiga kofi Macron, alitamka kauli ya 'Montjoie Saint-Denis!', inayojulikana kama nara iliyotumiwa na wafalme wa Ufaransa katika vita vya karne ya 11 na 12.

Alimaliza kauli yake kwa kusema 'Down with Macronism'.

Baada ya kutembelea shule ya upili ya usimamizi wa hoteli ya utalii katika jiji la Tain-l'Hermitage, Macron alikuja ana kwa ana na umati uliokuwa ukimsubiri nyuma ya vizuizi kwa ajili ya kupeana mikono.

Mtu mmoja kutoka kwenye umati alikuja na kumpiga kofi Macron.

**TRT**

# Museveni ateua baraza la mawaziri 80

**Kampala,** UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amefanya uteuzi wa baraza jipya la mawaziri 31 na manaibu waziri 50.

Hatua ya Rais Museveni kuwateua wanawake wengi kwenye baraza lake la mawaziri ikilinganishwa na serikali zake za awali, imepokelewa kwa maoni mseto na mshangao na mashaka, baada ya kuteua wanawake 10.

Jessica Alupo, ambaye ni meja mstaafu wa jeshi, ameteuliwa kuwa Makamu wa Rais. Ni mwanamke wa pili katika historia ya nchi hiyo, kuteuliwa katika wadhifa huo, pia aliwahi kuhudumu kama Waziri wa Elimu.

Robinah Nabbanja, ofisa wa ngazi ya juu wa chama tawala, ameteuliwa kuwa Waziri Mkuu na kiongozi wa shughuli za serikali bungeni. Alikuwa naibu waziri wa afya.

Rebecca Kadaga, wakili na mwanasiasa wa zamani ambaye hadi uteuzi wake katika baraza la mawaziri alikuwa spika wa bunge amepewa wadhifa wa naibu waziri mkuu wa kwanza. Pia amepewa jukumu kusimamia masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Baraza hilo la mawaziri pia linajumuisha maofisa wapya kutoka jeshini. Kamanda Mkuu wa sasa wa Majeshi, Jenerali David Muhoozi, ndiye naibu waziri wa mambo ya ndani. Jenerali Muhoozi pia anawakilisha jeshi bungeni.

Mmoja wa mawakili wa kibinafsi wa rais, Kiryowa Kiwanuka, ameteuliwa kuwa Mawanasheria Mkuu.

Sam Kuteesa, ambaye amekuwa Waziri wa Uganda wa Mambo ya Nje kwa muda mrefu, ameondolewa katika baraza la mawaziri.

**BBC**



Winchi ikilinyanyua basi lililoharibiwa baada ya kugongana na gari la kunyanyulia mizigo eneo la Kanpur Nagar, Kaskazini mwa Jimbo la Uttar Pradesh, nchini India, juzi, huku watu 17 wakipoteza maisha na wengine kujeruhiwa. **PICHA: XINHUA**

# Kenya kufunga maelfu nambari za siri walipakodi wasiowajibika

**Nairobi,** KENYA

MAMLAKA ya Mapato Kenya (KRA), inatarajiwa kuzifungia jumla ya nambari za siri 66,269 za kulipa kodi ambazo hazitumiki kufikia leo, ripoti za vyombo vya habari zimesema .

Wamiliki wa nambari hizo za siri za kulipa kodi ambao ni pamoja na watu binafsi na mashirika ya biashara, huenda wakafutiwa usajili malipo ya ushuru wa bidhaa.

Walipa kodi watakaoathiriwa, watazuiwa kutoza ada ya ushuru wa bidhaa katika biashara zao na huenda wakakabiliwa na vikwazo vingine vya utozaji ushuru.

Hatua kama hiyo pia itachukuliwa dhidi ya watu ambao hawajakuwa wakijaza fomu ya kuthibitisha wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria.

"Kufutiwa kwa jukumu la kulipa ushuru wa bidhaa ni mpango unaoendelea, utawaathiri walipa kodi ambao hawatajaza fomu ya kila mwezi ya kuthibitisha wamelipa ushuru wa bidhaa au wale ambao hawaoneshi jinsi walivyolipa ushuru huo kila mwezi miongoni mwa mambo mengine," KRA ilisema katika taarifa yake kwa umma.

**BBC**




# WACHEZAJI BRAZIL WAPINGA, WAKUBALI COPA AMERICA

**BRASILIA, Brazil**

KIKOSI cha Brazil kimesema "hatuungi mkono" michuano ya Copa America, lakini hawatagomea kucheza kwenye mashindano hayo yanayoanza mwishoni mwa wiki hii.

Copa America imepangwa kuanza Jumapili hii, lakini mashindano hayo yamegubikwa na kivuli cha utata baada ya Shirikisho la Soka la Amerika Kusini (CONMEBOL), kuyahamishia Brazil.

Yakiwa yameahirishwa mwaka 2020 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Copa America ilipangwa kuandaliwa na nchini mbili za Colombia na Argentina, ingawa yaliondolewa kwenye nchini hizo kwa sababu ya COVID-19.

Brazil walipewa haki ya kuandaa mashindano hayo, licha ya nchini hiyo kuwa kwenye hali mbaya zaidi ya maambukizo ya corona.

Nahodha 'Selecao' hao, Casemiro, amebainisha kuwa timu yote inapinga mashindano hayo kufanyika kwenye ardhi yao, lakini hawatayagomea.

Baada ya Neymar na Lucas Paqueta kuiongoza Brazil kushinda mabao 2-0 kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar dhidi ya Paraguay Jumanne, kocha wa kikosi hicho, Tite alisema watacheza tu.

"Kwa sababu tofauti, mashindano haya hayakuzingatia ubinadamu, hatujaridhishwa na Copa America namna CONMEBOL ilivyoamua," walisema wachezaji wa Brazil.

Brazil ambayo ndio bingwa mtetezi wa michuano hiyo atafungua dimba dhidi ya Venezuela jijini Brasilia, Jumapili hii.

Kikosi hicho cha kocha, Tite, Brazil kimepangwa Kundi B pamoja na Colombia, Peru, Ecuador na Venezuela.

## WAKALA WA HAKIMI AKANA KUTETA NA PSG

**MILAN, Italia**

WAKALA wa Achraf Hakimi, Alejandro Camano, amesema hakuna makubaliano yoyote kati ya mchezaji huyo na Paris Saint-Germain juu ya uhamisho wa kutoka kwa mabingwa wa Serie A, Inter kwenda kwa miamba hao wa Ligue 1.

Hakimi aliisaidia Inter kutwaa taji lao la kwanza la Scudetto kwa kipindi cha miaka 10 msimu huu, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco, amekuwa akihusishwa na PSG kutokana na matatizo ya kifedha yanayoikumba Inter.

Huku Inter ikijaribu kupunguza gharama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Hakimi, Romelu Lukaku, Lautaro Martinez na Alessandro Bastoni wanaweza kuuzwa baada ya kuondoka kwa kocha, Antonio Conte.

PSG imeripotiwa kwamba ilitoa ofa ya Euro milioni 60 ambayo ilikataliwa na Inter ambao wanataka angalau Euro milioni 80 lakini Camano amekanusha mazungumzo na miamba hao wa Ufaransa.

"Hakujakuwa na makubaliano na PSG, hakuna chochote kwa sasa," alisema Camano akiiambia FCInter1908.

"Hatuna makubaliano na klabu hiyo ya Ufaransa kuhusu makubaliano binafsi. Yeye ana furaha kucheza pale Inter."

Mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Chelsea pia wameripotiwa kwamba wanawania kumsajili Hakimi, ambaye pia amekuwa akihusishwa na mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich.




## CEBALLOS HANA MPANGO NA BARCA

**MADRID, Hispania**

DANI Ceballos anapanga kufanya mazungumzo na Real Madrid kuhusu majaliwa yake yake, lakini uhamisho wa kwenda Barcelona kamwe hauwezi kuwa chaguo la kiungo huyo.

Ceballos alionyesha kiwango cha kuvutia katika msimu wake wa kwanza wa mkopo kule Arsenal, lakini hakuwa na kiwango kizuri msimu huu wa 2020-21.

Katika mechi 40 alizocheza kwenye mashindano yote, ametoa pasi za mwisho tatu na kutengeneza nafasi 41.

Wakati Carlo Ancelotti akiwa ameteuliwa kuwa kocha mpya wa Madrid, Ceballos anatarajia mambo yatakuwa tofauti kwake na kwa namna alivyochukuliwa na kocha Zinedine Zidane.

Ingawa malengo yake ni kutaka kucheza Madrid, lakini anatambua kwamba, majaliwa yake yanaweza kuwa sehemu nyingine kabisa.

"Ancelotti ndio kwanza kawasili, tunahitaji kuzungumza," alisema akiiambia redio ya Cadena Ser.

"Nafikiri mwaka huu nimekuwa mwenye wakati mgumu. Nafikiri ni wakati wa kutumika kwenye klabu kwa mkataba wa muda mrefu na kuwa na wakati wa kuonyesha kiwango changu.

"Barcelona? Hapana, hicho si kipaumbele changu, mimi nafikiria zaidi kubaki Real Madrid na si vinginevyo."

## HABARI MICHEZO




# HAZARD PASUA KICHWA UBELGIJI

**BRUSSLES, Ubelgiji**

EDEN Hazard alicheza dakika 10 tu katika mechi ya mwisho ya kirafiki ya Ubelgiji kabla ya mashindano ya Euro 2020, lakini kocha Roberto Martinez, amesisitiza kuwa lengo lao ni kumuona akiingia uwanjani.

Kutokana na misimu miwili aliyokuwa akisumbuliwa na majeraha pale Real Madrid, Hazard alitokea benchi dakika ya 82 ya mchezo dhidi ya Croatia katika ushindi wa 1-0 na kucheza mechi yake ya kwanza kwa Ubelgiji tangu Novemba 2019.

"Lengo la Eden ni yeye kuwa uwanjani," Martinez aliuambia mkutano wa waandishi wa habari baada ya mchezo.

"Ilikuwa karibu hatua ya kisaikolojia. Dakika hazikujali. Sasa atalazimika kupata dakika zaidi. Hatua inayofuata itakuwa kwenye mazoezi. Lazima achukue hatua hiyo mbele bila hatari, kwa njia salama.

"Ni ngumu kusema ni lini atakuwa tayari, nadhani inategemea mambo mengi. Kilicho muhimu ni kwamba yuko sawa kiafya sasa. Nataka kumuona Hazard akiwa na furaha, akiwa na tabasamu usoni, na kufanya tofauti."

## DE BEEK SASA KUIKOSA EURO 2020

**AMSTERDAM, Uholanzi**

NI muendelezo wa msimu mbaya kwa kiungo wa Mancheester United na timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek, baada ua kuondolewa kwenye kikosi hicho cha timu ya taifa.

Na sasa majeraha yamemfanya Van de Beek kukosa kwenye michuano ya Euro 2020 inayoanza kesho, Ijumaa.

Van de Beek alijiunga na United Agosti 2020 akitokea Ajax na hakuwa na wakati mzuri pale Old Trafford.

Usajili wa Van de Beek haukutegemewa na wadau wengi wa soka hasa mashabiki wa United na mpaka msimu wa 2020/21, unahitimishwa, alikuwa ni mchezaji asiye na namba kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Pengine mashindano haya ya Euro 2020 ndiyo yalikuwa sehemu ya Van de Beek kuonyesha uwezo wake wa kucheza soka la kiufundi, lakini mambo yamekuwa tofauti.

Kocha wa Uholanzi, Frank De Boer, amethibitisha kuondolewa kwa mchezaji huyo kwenye kikosi cha timu yake na hana mpango wa kuita mchezaji wa mbadala kwenye nafasi hiyo.

Van de Beek alikuwa kwenye benchi katika mchezo dhidi ya Scotland licha ya kutokuwapo kwenye mazoezi ya timu hiyo sambamba na wachezaji wengine.

## LIVERPOOL YATUMA OFA KWA PELLEGRINI



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imewasilisha ofa ya awali ya pauni milioni 26 kwa nyota wa AS Roma, Lorenzo Pellegrini, wakati wakitafuta mbadala wa Georginio Wijnaldum.

Pellegrini amemvutia kocha Jurgen Klopp kwa kufanya kwake vizuri msimu uliopita, na anaamini atakuwa mrithi mzuri wa Wijnaldum anayeondoka klabuni hapo.


Nyota huyu aliwafungia Roma mabao 11 na kutoa usaidizi wa mabao mengine tisa kwa michuano yote msimu uliopita.

Akiwa na mwaka mmoja tu uliosalia kwenye mkataba wake, inaaminika kuwa Roma watalazimika kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 kwenye dirisha la uhamisho la msimu huu wa majira ya joto.

Kwa mujibu wa Corriere dello Sport, Liverpool imekuwa klabu ya kwanza kuwasilisha ofa ya kumsajili nyota huyo, na hili ni jaribio kwa Roma ambao wanaonekana bado wanamhitaji.

Hata hivyo, klabu hii ya Serie A chini ya kocha mpya, Jose Mourinho, inatarajiwa itaendelea kuwa na mchezaji huyo.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KANE, GREALISH KUONDOA NYOTA MANCHESTER CITY

●●● Lakini dau linalotakiwa na klabu zao za Tottenham na Aston Villa linaweza...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City watauza wachezaji kadhaa ili kupata kiasi cha pauni milioni 70 kwa ajili ya kumsajili nyota wa Tottenham Hotspur, Harry Kane na mkali wa Aston Villa, Jack Grealish, limeripoti gazeti la Daily Mail.

Man City malengo yake ni kuhakikisha kwamba wanalibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kulikosa msimu huu na njia pekee ni kusajili nyota wengine.

**City imekuwa ikihusishwa na nyota hao wa England, Kane na Grealis ili kuimarisha kikosi chao tayari kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.**

Lakini kiasi kinachotakiwa na klabu zao za Tottenham na Aston Villa kwa ajili ya kuwaachia wachezaji hao kinaweza kikaonekana kikwazo. Huku Sergio Aguero akiwa ameondoka, City na kocha Pep Guardiola wanataka kutafuta nyota ambao watawasaidia kwenye safu ya ushambuliaji pale mbele.

Wachezaji wa kikosi cha kwanza Raheem Sterling, Gabriel Jesus, Ilkay Gundogan, Bernardo Silva na Riyad Mahrez hawa wote wanaonekana bado kuwa na maisha hapo kwenye dimba la Etihad.

Lakini nyota wenye vipaji kama Yangel Herrera, Ivan Ilic, Jack Harrison, Pedro Porro na Lukas Nmecha, ambao wamekuwa wakicheza kwa mkopo sehemu nyingine, wanaweza kuuzwa.

Silva amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kwenda Atletico Madrid kwa kubadilishana na Saul Niguez, huku Juventus ikiripotiwa kumkodolea macho Gundogan.

## KWA UFUPI

**BELLIRIN KWENDA JUVE**
JUVENTUS wanamtaka Hector Bellerin na huenda wakamuachia tena kiungo wa kati wa Wales wa mwenye umri wa miaka 30, Aaron Ramsey, katika mkataba wa kubadilishana wachezaji na Arsenal. (***Sport***)

**SANTO AKARIBIA PALACE**
KOCHA wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo, anakaribia kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Crystal Palace. (***Telegraph***)

**PELLEGRINI HUYO LIVERPOOL**
LIVERPOL wametangaza dau la pauni milioni 25.8 kumnunua nahodha wa AS Roma na kiungo wa kati wa Italia, Lorenzo Pellegrini mwenye umri wa miaka 24, kuchukua nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 30. (***Corriere dello Sport, via Sun***)

**NIGUEZ KUMBADILISHA SILVA**
KLAbu ya Atletico Madrid imemtoa kiungo wa kati wa Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26 kwa Manchester City ili wampate mshambuliaji wa Ureno, Bernardo Silva, 26. (***Times***)

**HAALAND AITAKA CHELSEA**
NYOTA wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, anapania kujiunga na Chelsea na yuko tayari kusubiri kwa mwaka mmoja kuhamia Stamford Bridge. (***Telegraph***)

**MINAMINO KURUDI SOUTHAMPTON**
MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Japan, Takumi Minamino, amehusishwa na tetesi za kurejea Southampton ambako alikuwa kwa mkopo msimu uliopita baada ya kocha Ralph Hasenhuttl, kuulizia mpango wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26. (***HampshireLive***)

**CEBALLOS AITAKA LALIGA**
NYOTA wa Hispania, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 24, amesema anataka kurejea LaLiga msimu ujao baada ya mkataba wake wa mkopo Arsenal kutoka Real Madrid kumalizika. (***Cadena SER, via Evening Standard***)

**NEVES ANUKIA ARSENAL**
ARSENAL wamefanya mazungumzo na Wolves kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves, wakati 'Washikabunduki' hao wakijiandaa kupanga orodha ya wachezaji wanaopigiwa upatu kujaza nafasi ya Granit Xhaka mwenye umri wamiaka 28. (***Goal***)

**BAYERN KWA HUDSON-ODOI**
BAYERN Munich wamefufua mkakati wa kumsaka winga wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20. (***Times***)

**POTTER AITAKA EVERTON**
KOCHA wa Brighton, Graham Potter bado anagombea kuwa kocha mpya wa Everton baada ya Carlo Ancelotti kuondoka. (***Athletic***)

**MILAN HESABU KWA DIAZ**
AC Milan wamefahamishwa kwamba kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 21 kwa mkataba wa kudumu kutoka Real Madrid, kutawagharimu Euro milioni 26.(***Goal***)

**HODGSON AIKATALIA WEST BROM**
ROY Hodgson amekataa ombi la West Brom la kumtaka awe kocha wao mpya. (***Football Insider***)

# SBL YAITABIRIA STARS USHINDI DHIDI YA MALAWI JUMAPILI

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya mechi ya kimataifa ya kirafiki kati ya Taifa Stars na timu ya Taifa ya Malawi maarufu kwa jina la 'The Flames', wadhamini wakuu wa Taifa Stars, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), wameitabiria ushindi.

Utabiri wa ushindi wa Taifa Stars dhidi ya Malawi unakuja baada ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kim Paulsen kutangaza kikosi cha wachezaji 27 walioingia kambini tangu Juni 5, mwaka huu kujiandaa na mechi hiyo iliyopo kwenye Kalenda ya FIFA ambayo itakayochezwa Jumapili wiki hii majira saa 10:00 alasiri katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salam.

Akizungumza wakati wa kutangaza kikosi hicho, hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Kocha Paulsen alisema mechi dhidi ya Malawi ni muhimu kwa kuwa itaisaidia Stars kujipima nguvu wakati ikijiandaa kwa ajili mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwaka 2022.

Kim Paulsen alisema amewaita wachezaji mchanganyiko wakiwamo chipukizi na wakongwe ambao baadhi yao wanacheza soka la kulipwa mataifa mbalimbali duniani, lengo likiwa ni kutengeneza kikosi imara ambacho hakitakuwa kinabadilika mara kwa mara.

Meneja wa Bia wa SBL, Wankyo Marando, alisema kampuni hiyo kama mdhamini mkuu wa timu ya Taifa Stars, wana imani kubwa na kikosi kilichotangazwa na Poulsen, hivyo ni wakati wa Watanzania kujitokeza kwa wingi kwenda kuishangilia timu yao.

"Tunayo imani kubwa na kikosi alichokitaja kocha mkuu. Hatuna shaka kuwa kikosi kitakwenda kufanya vizuri katika mechi hiyo muhimu ya kujipima nguvu dhidi ya Malawi," alisema.

Wankyo alisema SBL ambayo inaidhamini Taifa Stars kupitia bia yake ya Serengeti Lager, itaendelea kuiunga mkono timu hiyo ya taifa ili kuhakikisha inafanya vizuri katika mechi zake na kuwapa raha mashabiki wa soka nchini.

"Chapa ya Serengeti ni mdau mkubwa wa michezo hapa nchini na tunaona furaha kuchangia maendeleo ya michezo na tunaahidi kuendelea kuhamasisha na kuchangia maendeleo ya sekta hii ambayo pia huwaleta watu pamoja," alieleza.

Mwaka jana, Bia ya Serengeti Premium Lager iliingia mkataba wa miaka mitatu na TFF na kuwa mdhamini mkuu wa Taifa Stars kwa makubaliano ya kutoa kiasi cha Sh. bilioni tatu katika kipindi hicho cha mkataba. Mkataba huo ulikuja baada ya kumalizika ule wa awali ambao pia ulikuwa ni wa miaka 3 uliosainiwa mwaka 2017. SBL pia ni mdhamini mkuu wa Ligi ya Wanawake ikiwa ni mara ya kwanza kwa ligi hiyo kupata mdhamini tangu ianze na kuifanya kampuni hiyo kuwa mdhamini wa kwanza wa ligi hiyo.



Makipa wa Taifa Stars, Aishi Manula na Juma Kaseja (nyuma), wakiwa mazoezini katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi, kujiandaa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Malawi utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii. Pembeni ni beki wa kulia wa timu hiyo, Shomari Kapombe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dk. Mwinyi akunwa na mkakati Small Simba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameupongeza utayari wa uongozi wa Klabu ya Small Simba wa kutaka kurejesha hadhi ya michezo visiwani hapa.

Rais Dk. Mwinyi ameyasema hayo jana Ikulu mjini Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na uongozi wa Klabu ya Small Simba, ambayo siku za nyuma iliwika katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar.

Katika maelezo yake, Rais Dk. Mwinyi, alisema moja kati ya ahadi zake katika kampeni za uchaguzi mkuu, ilikuwa ni kurejesha hadhi ya michezo kama au zaidi ya ilivyokuwa katika uongozi wa serikali ya za awamu zilizopita, jambo ambalo litafanywa na wadau wa michezo na serikali jukumu lake ni kuweka mazingira mazuri.

Rais Dk. Mwinyi alieleza kwamba mafanikio katika sekta ya michezo, hayawezi kupatikana iwapo hakutowekwa mazingira mazuri katika sekta hiyo, hivyo Serikali ya Awamu ya Nane, itaendelea kushirikiana na wadau wote wenye azma ya kuiimarisha sekta ya michezo ili kuhakikisha inaimarika.

Alitoa pongezi kwa uongozi huo kutokana na mawazo yao ambayo yanaendana na yale ya serikali yake kuanzia chini kwa kuanzisha kituo cha kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana huko Fuoni Kibondeni jambo ambalo ni jema na aliliunga mkono huku akisisitiza kwamba nchi zote zilizofanikiwa katika soka duniani zimeanzia na vituo vya mafunzo na kuibua vipaji vya vijana wakiwa wadogo.

Alisema kwa vile tayari timu hiyo imeshapatiwa eneo la kudumu la kufanyia shughuli zao, ni jambo jema ambapo hatua inayofuata ni kuhakikisha linakuwa na miundombinu inayotakiwa hasa ikizingatiwa kwamba tayari wameshalifanyia upembuzi yakinifu.

Rais Dk. Mwinyi aliunga mkono maelezo ya uongozi huo kwamba michezo ni biashara na si burudani peke yake hivyo, ni vema klabu zote zikaendeshwa kibiashara hatua ambayo itasaidia kutoa ajira pamoja na kuongeza ari ya vijana kujinga katika michezo.

# Nandy ala shavu la maana TTCL

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL), limetia saini ya makubaliano na Msanii wa Muziki wa Kizazi Kipya, Faustina Mfinanga, maarufu Nandy ya kuwa mdhamini mkuu wa Tamasha la Nandy 2021.

Hafla ya makubaliano hayo ilifanyika Ofisi za TTCL Kijitonyama, Dar es Salaam ambako uongozi wa EASTWAVE MARKETING ambao ndiyo waandaaji wa Tamasha hilo waliomba TTCL kushirikiana nao katika kufanikisha tukio hilo nchini na Afrika.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Biashara kutoka TTCL, Vedastus Mwita, alisema kuwa baada ya mchakato wa kibiashara kukamilika, TTCL imekuwa mdhamini mkuu wa tamasha hilo ambalo kuanzia sasa litaitwa 'TTCL Nandy Festival 2021- Watakaa Tu'.

Tamasha hili litafanyika katika mikoa 10 ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Rukwa, Kigoma, Shinyanga, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Zanzibar huku matarajio yakiwa ni wananchi wa mikoa hiyo na visiwa vya Zanzibar kupata burudani ya muziki yenye ubora na kiwango cha kimataifa.

Kwa upande wa Nandy, alisema TTCL kujitoa na kuwa mdhamini mkuu si jambo dogo, akilishukuru shirika hilo kwa kuona umuhimu wa kutumia tamasha lake kuwarudisha Watanzania nyumbani kupitia burudani atakayoitoa katika mikoa iliyoandaliwa.

# Biashara yapania kuishika Yanga FA

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Klabu ya Biashara United, Abdulmajid Mangalu, amesema kwa kushirikiana na wachezaji wenzake, watapambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wao wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, utakaopigwa kati ya Juni 25-27, mwaka huu katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Mara, nahodha huyo aliweka wazi mikakati yao hiyo na kuahidi kuipigania timu yake ili kushinda na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Tunaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Yanga katika mchezo wetu wa nusu fainali, lengo langu ni kuhakikisha timu yangu inasonga mbele kwenye michuano hiyo," alisema Mungalu.


Nahodha huyo alisema anatambua ugumu wa mchezo huo, hivyo wana kila sababu ya kujituma kufanya mazoezi ili wawape burudani mashabiki wao ambao aliwaomba kuendelea kuwaunga mkono.

Aidha, alisema kwa sasa mkataba wake na klabu hiyo umemalizika, hivyo yupo tayari kwenda kuitumikia yoyote itakayompa maslahi mazuri.

# Michezo

Alhamisi Juni 10, 2021

Nipashe

KANE, GREALISH KUONDOA NYOTA MAN CITY

HABARI UK 22

## NGOME KALI...



Mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, akipata upinzani mkali kuipenya ngome ya Bulgaria wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Stade de France juzi. Mabao yakifungwa na Antoine Griezmann dakika ya 29 na Olivier Giroud (dk. 83 na 90). **PICHA: MTANDAO**

# KARIA AZIDI KUPATA WAPINZANI URAIS TFF

●●●Wengi wataka kiti chake, mchambuzi maarufu wa soka naye ndani, Kamati ya Utendaji napo...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

IKIWA jana ni siku ya pili tu tangu dirisha la kutolewa fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), lifunguliwe rasmi, mbio hizo zimepamba moto na tayari jumla ya wagombea tisa wamejitokeza huku watano kati yao wakiwania kiti cha urais.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, mbali na kiti cha urais, nafasi zingine zinazowaniwa katika uchaguzi huo utakaofanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu, ni sita za Wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema hadi kufikia jana jumla ya wanafamilia tisa wamechukua fomu kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa shirikisho hilo katika Ofisi za TFF na watano kati yao wakiwa ni kiti cha urais.

"Nafasi ya urais waliojitokeza hadi kufikia leo (jana) saa 10 jioni ni Deogratius Mutungi, Evans G. Mgeusa, Oscar Oscar, Wallace John Karia na Zahor Mohammed Haji.

"Kwa upande wa nafasi ya Kamati ya Utendaji ni Lameck, Nyambaya, Liston Katabazi na Michael Petro (Kanda namba 1- Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara na Pwani), mwingine ni Khalid Abdallah (Kanda namba 2- Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga)," Ndimbo alisema.

Karia ambaye anamaliza muda wake, yupo jijini Mwanza kwa majukumu yake ya kikazi ya shirikisho hilo, lakini juzi alichukuliwa fomu ya kutetea nafasi hiyo na Mwenyekiti wa zamani wa Klabu ya Simba, Swedi Mkwabi, katika Ofisi za TFF jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa Oscar Oscar, ambaye ni mwandishi wa habari na mchambuzi wa soka katika Kituo cha Redio EFM, baada ya kuchukua fomu jana, aliwaambia wanahabari wenzake kwamba ameamua kugombea nafasi hiyo ya urais kwa lengo la kuhakikisha maendeleo ya soka yanakwenda mbele zaidi.

"Nimeamua kuchukua fomu hii kwa sababu nina lengo la kuongoza mpira wa dunia, nimefikia uamuzi huu ninataka kuwa miongoni mwa watu wenye uamuzi wa kuhakikisha mpira wetu unasonga mbele," alisema Oscar.

Alisema moja ya uzoefu wake katika uongozi wa soka, kabla hajawa mchabuzi, aliwahi kufanya kazi akiwa miongoni mwa waajiriwa wa Klabu ya Azam kipindi ambacho timu hiyo ilitwaa ubingwa wa Ligi Kuu mwaka 2014.

Jina lingine linalosubiriwa kwa hamu na wadau wa soka nchini ni la Mwenyekiti wa zamani wa Klabu ya Yanga na Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba, ambaye mapema wiki hii alionyesha nia ya kuingia katika mbio za kiti cha urais wa shirikisho hilo.

Hiyo ni baada ya juzi Tarimba kumwambia mwandishi wetu: "Hizo taarifa zipo, watu wengi sana walikuwa wananiomba ama wananishauri, sijui kati haya mambo mawili, lakini watu wanalizungumza hilo suala. Siwezi kusema ndiyo ama hapana, lakini kama Mtanzania na kama wenzangu wananiona na mimi najiona kama nafaa, ila hadi sasa sijafanya uamuzi."

Dirisha la kutolewa kwa fomu hizo linatarajiwa kufungwa rasmi Jumamosi wiki hii.

## MANYAMA AISHTUA RUVU KUTUA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ruvu Shooting imeeleza kushangazwa na taarifa za beki wao wa kushoto, Edward Charles Manyama, kumalizana na mabingwa wa nchi, Simba, kwa ajili ya kuitumikia msimu ujao.

Kwa mujibu wa taarifa za ndani kutoka kwa watu wa karibu wa mchezaji huyo, tayari Manyama anadaiwa kumalizana na Klabu ya Simba, ambayo imewazidi ujanja watani zao, Yanga, waliokuwa wameanza naye mazungumzo na kufikia pazuri.

Ofisa Habari wa klabu hiyo Masau Bwire, amesema tangu jana asubuhi ameona taarifa hizo zikienea, lakini wao kama Ruvu Shooting wanachofahamu ni kwamba, mchezaji huyo yupo kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars.

"Tunavyojua sisi ni kwamba ligi bado haijaisha na mchezaji hawezi akahama wakati bado inaendelea. Manyama ni mchezaji wetu na ataendelea kuitumikia Klabu ya Ruvu Shooting mpaka ligi itakapokwisha. Na sasa ninapozungumza ni kwamba tumemruhusu akajiunge na timu ya Taifa, Taifa Stars na si vinginevyo," alisema Masau.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Haji Manara, alisema hakuna kipindi kigumu kama hiki kinachokuja cha usajili.

Alisema ni kipindi ambacho mara nyingi kunakuwa na tetesi nyingi ambazo zinawapa presha wanachama na mashabiki wa klabu mbalimbali.

Manara aliwakumbusha wanachama na mashabiki wa Simba mfumo wao wa utoaji taarifa ni ule ule wanaoufahamu. Simba kwa misimu miwili, imekuwa ikisajili wachezaji kimyakimya, halafu wanawatambulisha kwenye mtandao wao wa kijamii majira ya saa saba mchana. Manyama anaichezea Ruvu Shooting kwa mkopo akitokea Namungo FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002